# Nipashe

Jumatano Mei 20, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580236

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710




## Ajiua kwa risasi kushindwa kulipa mil. 100/- za benki

UKURASA 16



Hatua kujiangalia Rais Uhuru, Ruto kukwepa Kenya ya 2007

siasa

HABARI BORA NA KAMILIFU

Uwezo, maajabu walinzi 12 wa Rais Kim Jong-un-2

BALOZI MAHIGA

Mbobezi wa UDSM aliyetumika UN kuleta amani maeneo korofi

UKURASA 11

# Tanzania yafunga mpaka na Kenya

## BALOZI wa nchi hiyo atoa ufafanuzi kuhusu uhusiano...*Endelea ukurasa 2*



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigela

Balozi wa Kenya nchini, Dany Kazungu

## Mch. Msigwa amwangukia Kinana

UKURASA 2

## MIL. 780/- ZASIMAMISHA WATUMISHI WA TEMESA

UKURASA 8

## BAA LA CORONA



Katika kipindi hiki cha kujilinda na ugonjwa wa Covid-19, fanya mazoezi ya viungo ya kawaida angalau dakika 150 kila siku kwa wiki nzima, au dakika 75 za mazoezi ya nguvu yakiwamo ya misuli mara mbili kwa wiki. WHO

* **Epuka mikusanyiko ya watu**
* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store


**MICHEZO** NDEMLA ONDOKA SIMBA- MENEJA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Mwandishi wa habari wa TBC, Monica Lyampawe, akipata maelezo kutoka kwa mkazi wa Kijiji cha Kambala, Ruben Olenata, kuhusu mimea inayotumika kujifukiza ili kuupa mwili kinga dhidi ya magonjwa mbalimbali, wakati waandishi wa habari wa mkoa wa Morogoro, walipofika kijijini hapo kikazi, juzi. **PICHA: FRANK KAUNDULA**

# Tanzania yafunga mpaka Horohoro

**Na Waandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigela, amefunga mpaka wa Horohoro na kuzuia magari yanayotoka na kuingia nchini kutoka Kenya, baada ya madereva 19 kutoka nchi hiyo jirani kupimwa na kubainika kuwa na maambukizo ya virusi vya corona.

Shigela alitoa amri hiyo jana alipotembelea mpaka huo na kuzungumza na madereva wa magari ya mizigo wa upande wa Tanzania yaliyokwama baada ya kuzuiwa Mpaka wa Lungalunga na Serikali ya Kenya, iliyowataka kupimwa corona na kukaa siku tatu kusubiri majibu ya vipimo.

"Mimi nikiwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, ninayo mamlaka ya kusimamia mpaka wa Horohoro niliokabidhiwa kuusimamia. Iwapo ninaona mambo hayaendi sawa, ni lazima nichukue hatua," alisema.

Shigela aliviagiza vyombo vya usalama kuhakikisha raia wa Kenya hawaingii nchini kupitia njia za panya kama walivyozoea baada ya kuwekewa vizuizi kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Kwa upande wao madereva hao waliozuiliwa kuvuka mpaka wa Lungalunga, walilalamikia uamuzi huo wa mkuu wa mkoa wakisema bidhaa walizobeba ziko mbioni kuharibika kwa kuwa nyingi ni vyakula kama nyanya na ndizi.

**UFAFANUZI WA KENYA**

Wakati Shigela akitangaza uamuzi huo, Balozi wa Kenya nchini, Dany Kazungu, alisema jana kuwa Kenya haijawazuia madereva wa Tanzania kuingia katika nchi hiyo, isipokuwa imeweka masharti ya kuhakikisha wanaoingia ni wale waliothibitika kuwa hawajaambukizwa virusi vya corona.

Kazungu alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati alipozungumza na waandishi wa habari.

"Watu wanazungumza kuhusu kufungwa kwa mpaka, lakini hawaongei yote. Rais (Uhuru) Kenyatta aliposema kuhusu mpaka, alimaanisha kwamba hata dereva Mtanzania anayepimwa na kuonekana yuko 'negative' (hana maambukizo), aingie kwenye gari, alete mzigo wake Kenya bila kushurutishwa.

"Pia, Rais alisema dereva Mkenya hawezi kutoka Kenya bila kupata kibali kwamba amepimwa na yuko sawa, ili asiende kuwaambukiza Watanzania au Waganda au wengine katika nchi hizi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, ndiyo vilevile tumesema pia dereva wa Tanzania naye akifika hapa, apimwe kama yuko sawa aingie kwenye gari apeleke mizigo Kenya.

"Hii hatua ambayo Kenya imeichukua siyo kwa sababu ya Tanzania, ni kwa sababu tunaangazia yule adui yetu sote ambaye ni corona, na wahenga wanasema 'vita vya panzi ni furaha ya kunguru'. Kunguru ndiye huyu kirusi, tuvute subira, sisi ni watu wanaopendana, wazalendo.

"Rais Kenyatta anasema haiangalii Tanzania kama jirani, anaiangalia kama ndugu na dada, katika moyo wake anataka tuwe na uelewano zaidi kwa sababu ni wamoja. Wito wetu hapo ni kwamba, tunaomba tuwe na subira, tuwaache viongozi wetu walitatue hili jambo," alisema.

Balozi Kazungu alisema tayari amezungumza na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamagamba Kabudi, ambaye amemwahidi kuzungumza na Waziri wa Mambo ya Nje wa Kenya.

"Nimezungumza na waziri wangu wa masuala ya nje, pamoja na Profesa Kabudi ambaye amesema mwisho wa wiki ataongea na mawaziri wenzake kule Kenya waweke mambo vizuri, kirusi kisiwe sababu ya sisi kugongana, ninawaomba Watanzania tuweke hisia chini, viongozi watatuelekeza njia nzuri ya kufuata," alisema.

Balozi Kazungu alikumbusha kuwa Tanzania inapakana na nchi nyingi, lakini imepakana katika eneo kubwa zaidi na Kenya, hivyo kuna umuhimu nchi hizo mbili kuhakikisha zinaweka mambo yao vizuri.

"Na ijulikane kwamba Tanzania na Kenya ndiyo miamba ya uchumi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kati, kwa hiyo nchi hizi mbili zinaposhirikiana zaidi, ndiyo uchumi wa eneo hilo zima unaposimama vizuri, lakini sisi tukianza kuyumba, tunayumbisha na wengine," alisema.

Balozi huyo alisema nusu ya biashara inayofanyika Afrika Mashariki, inafanyika kati ya nchi hizo mbili na ndiyo nguzo ya uchumi wa jumuiya.

Kazungu alisema undugu na urafiki wa nchi hizo mbili utaendelea kuwapo na ndiyo maana Kenyatta alikuwa wa kwanza kusafiri na ndege yake kwenda kumsalimia Rais John Magufuli wilayani Chato mkoani Geita.

"Rais Kenyatta alikuwa amepanga kwamba siku ya sherehe za Muungano Aprili 26, mwaka huu aje Tanzania kusherehekea, na tulitarajia labda angekuwa na ziara ya wiki nzima kwa Tanzania Bara na Zanzibar ili kuzidi kuleta uwiano wa kufanya kazi pamoja," alisema.

Kuhusu waandishi wa habari wa Kenya waliokamatwa mpakani Namanga, Balozi Kazungu alisema tayari wamewasiliana nao na wamejitetea kwamba waliingia Tanzania bila kujua na kwamba suala hilo wameacha lishughulikiwe na Idara ya Uhamiaji ya Tanzania.

"Ni kweli waandishi wa habari wa Kenya walikamatwa, na tuliwasiliana nao wakasema kwamba wana kituo chao pia pale Namanga. Kwa hiyo, wakati wanafanya mahojiano pale, hawakujua kama wamekanyaga katika eneo la Tanzania. Sisi tumewaachia Uhamiaji, wao ndiyo wanashughulikia suala hilo kwa mujibu wa sheria za Tanzania," alisema.

*Imeandikwa na Hamida Kamchalla (TANGA) na Elizabeth Zaya (DAR)

# Mbunge Msigwa amwangukia Kinana

**Na Mwandishi Wetu**

MBUNGE wa Iringa Mjini, amemwomba radhi Katibu Mkuu mstaafu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana, kutokana na kauli za uongo alizowahi kuzitoa dhidi yake.

Katika nyakati tofauti, ndani na nje ya Bunge, Mchungaji Peter Msigwa aliwahi kutoa kauli za uzushi dhidi ya Kinana, akimtuhumu kujihusisha na ujangili na biashara ya nyara za serikali.

Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, mbunge huyo alisema tuhuma zote alizowahi kuzitoa dhidi ya Kinana bungeni na kwenye mikutano ya kisiasa nje ya Bunge, hazikuwa na ukweli wala ushahidi wowote.

"Ni dhahiri kwamba nimemkosea, nimemdhalilisha na kumkashifu ndugu yangu Abdulrahman Kinana. Nimekutana na kuzungumza naye kuhusu jambo hili na kumwomba radhi. Ninashukuru kwamba amekubali kunisamehe.

"Bila shaka mtakubaliana nami kwamba Kinana ni mzalendo, muungwana na mstaarabu ambaye kwa kweli hastahili kukashifiwa wala kudhalilishwa.

"Nitaendelea kumheshimu kama alivyodhihirisha ustahimilivu na uungwana wake kwangu, kwa familia yangu na kwa Watanzania," Mchungaji Msigwa alisema.

Mahakama Kuu ya Tanzania, kupitia kesi namba 108 ya mwaka 2013, ilimkuta Mchungaji Msigwa na hatia ya kuandaa na kutoa kashfa dhidi ya Kinana kwa malengo ya kisiasa, kumchafulia jina na kumshushia hadhi yake katika jamii; ndani na nje ya nchi.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari jana, Mchungaji Msigwa alisema kujutia kitendo chake hicho kwa kusema yeye ni binadamu na kukosea ni jambo la kawaida na kilichofanywa na Kinana kwenda kumshtaki mahakamani ni jambo la haki.

"Ninakiri mbele yenu kwamba tuhuma nilizozitoa mara kwa mara dhidi ya Ndugu Kinana hazikuwa na ukweli wala ushahidi wowote. Taarifa nilizopewa na kuzitumia hazikuwa zimefanyiwa utafiti, bali za kuungwaungwa na zenye malengo ya kisiasa na kizandiki.

"Hata hivyo, mambo kama haya hutokea katika maisha na sisi kama binadamu hutokea tukawakosea wenzetu. Inapotokea kuwakosea wenzetu, tunatakiwa kuwa tayari kuomba radhi na tunaowakosea nao kuwa tayari kusamehe," alisema.

Kabla ya kupeleka suala hilo mahakamani, Kinana kupitia kwa Wakili wake, Erick Sikujua Ng'maryo, alimtaka Mchungaji Msigwa kufuta kauli zake hizo na kuomba radhi hadharani kwa kuwa hazikuwa na ukweli wowote. Mbunge huyo alikataa kufanya hivyo na kusema yuko tayari kujitetea mahakamani.

Jaji Zainab Muruke aliyesikiliza na kuamua kesi hiyo, alisema kitendo cha wanasiasa kutoa kauli za kudhalilisha wenzao pasipo kuwa na ushahidi wala ukweli wowote ni "tabia mbaya" inayopaswa kukemewa.

"Kumekuwa na dhana kwamba siasa ni mchezo mchafu na kwamba kauli za kudhalilisha heshima na utu wa wengine zinakubalika kwenye majukwaa ya kisiasa. Hii si sahihi kwa sababu wanasiasa na viongozi wanatakiwa kuwa mfano wa kuigwa mbele ya jamii.

"Katika kutoa hukumu, Mahakama Kuu imetambua historia ya uongozi na utendaji uliotukuka wa Ndugu Kinana ambaye amewahi kushika nyadhifa mbalimbali za juu ikiwa ni pamoja na ubunge, uwaziri, Uspika wa Bunge la Afrika Mashariki, Ukatibu Mkuu wa CCM na majukumu mengine ya kiuongozi katika ukanda wetu huu na kimataifa.

"Imedhihirika wakati wa kusikilizwa kesi hii na kwa kuzingatia hoja zilizowasilishwa na pande zote mbili, tuhuma dhidi ya Kinana zilikuwa na lengo la kumchafua, kumdhalilisha na kumshushia heshima katika ngazi zake za kiuongozi na bila shaka zikiwa na msukumo wa kisiasa," Jaji huyo alisema.

Kesi hiyo ilinguruma Mahakama Kuu kwa miezi 36 kabla ya kutolewa hukumu, huku shauri lenyewe likisikilizwa mahakamani mara 84. Mchungaji Msigwa hakuwahi kufika mahakamani wala kuwasilisha mashahidi katika kesi hiyo aliyokuwa akitetewa na Wakili Peter Kibatala katika hatua za awali na baadaye Hekima Mwasepo.

HABARI KITAIFA

# Japan yaipa Tanzania bil. 3.45/- kukabili utapiamlo

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Japan imetoa Dola za Marekani milioni 1.5 (Sh. bil. 3.45) kwa Shirika la Mpango wa Chakula la Umoja wa Mataifa (WFP) kwa ajili ya kuunga mkono mradi wake wa miaka minne wa Boresha Lishe kwa maeneo ya vijiji vya Kanda ya Kati mwa Tanzania.

Mradi huo uliozinduliwa mwaka 2017 unalenga kuimarisha lishe kwa wanawake na watoto 30,000 kwa kuhamasisha mabadiliko chanya ya tabia za lishe, kuhimiza uzalishaji wa mazao mbalimbali ya chakula na ugawaji wa chakula lishe maalumu kwenye wilaya za Bahi na Chamwino kwa Mkoa wa Dodoma na wilaya za Ikungi na Singida Vijijini kwa Mkoa wa Singida.

"Kwa hapa Tanzania, Serikali ya Japan imekuwa ikitoa misaada kwa sekta mbalimbali," anaeleza Goto Shinichi, Balozi wa Japan nchini Tanzania.

"Mchango huu maalumu umetolewa kwa ajili ya wanawake na watoto wa vijijini, kwa ajili ya kuunga mkono kaulimbiu ya 'Hakuna kumwacha mtu nyuma' ya Mpango wa Maendeleo Endelevu wa 2030 kwa kuzingatia dhana ya msingi ya usalama wa mwanadamu. Msaada huu utasaidia kuboresha lishe na kuongeza kipato kwa makundi haya maalumu.

Taarifa iliyotolewa na WFP kwa vyombo vya habari jana, ilisema mradi wa Boresha Lishe unajikita kwenye kuongeza uelewa kuhusu; masuala ya lishe, upatikanaji wa vyakula mchanganyiko na usafi wa maji, mtu binafsi na mazingira (WASH).

Mradi pia unajengea uwezo jamii wa namna ya kuongeza uhakika wa lishe na chakula kwenye kaya kwa kufuga wanyama wadogo, kulima mazao mchanganyiko na kuwaunganisha kinamama kwenye vikundi vya Kuweka Akiba na Kukopa Vijijini (Vicoba), ili kusaidia upatikanaji wa mitaji.

Kwa ushirikiano na Japan, WFP inasambaza na kuweka vibanda vya huduma za umeme wa jua kwa vikundi 40 vya Vicoba vinavyosimamiwa na mradi huo. Vibanda hivyo vinatoa huduma za kuchaji simu na vifaa vingine vya umeme kwa malipo kidogo, na hivyo kuongeza kipato kwa Vicoba na wanachama wake.

"Kwa kupitia mradi wa Boresha Lishe, WFP inatumia mbinu ya sekta jumuishi kwa kugawa chakula lishe maalumu na kuhimiza mabadiliko chanya ya tabia za lishe huku ikiwawezesha wanajamii kuwa na shughuli mbalimbali za kiuchumi kwa ajili ya kuwaongezea kipato," anaeleza Michael Dunford, Mwakilishi Mkazi wa WFP Tanzania. "Kutokana na msaada wa serikali ya Japan, WFP inaimarisha lishe ya watoto na kutengeneza mustakabali mzuri wa baadaye wa jamii kwa ujumla."

Vile vile, ili kufanikisha kusambaza na kujenga vibanda vya kutolea huduma za umeme wa jua, WFP inafanya kazi kwa karibu na kampuni binafsi ya Kijapani, kwa lengo la kunufaika na utaalamu walionao katika kuendesha biashara hiyo kwa miaka mingi.

Mradi wa Boresha Lishe unafadhiliwa na Serikali ya Japan, Umoja wa Ulaya na WFP.

## Mahakama Kuu kuwaita kina Mbowe hukumu ikikamilika

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imesema hukumu ya rufani ya vigogo wanane wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), akiwamo Mwenyekiti Taifa, Freeman Mbowe itakapokuwa tayari walalamikaji na walalamikiwa watatumiwa wito.

Amri hiyo ilitolewa na Jaji Ilvin Mgeta baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Faraja Nchimbi akisaidiana na Salimu Msemo.

Akijibu hoja za walalamikaji, Wakili wa Serikali Msemo alidai kuwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, ilizingatia sheria ikiwamo kuchambua ushahidi wa pande zote mbili.

Hata hivyo, katika uchambuzi wake hakimu aliona ushahidi wa utetezi ni dhidi ya kujibu tuhuma za Jamhuri.

Aliendelea kujibu hoja za rufani, kwamba kuainisha ushahidi inategemea na mwandishi wa hukumu kwa kuwa kila mmoja ana namna yake ya kuandika, tofauti na wakili wa walalamikaji Peter Kibatala, alivyodai kuwa hukumu imeandikwa kwa kurasa chache.

Upande wa Jamhuri ambao ni walalamikiwa katika kesi hiyo, uliendelea kudai kuwa kutokuitwa OCD na Afande Dotto aliyekuwa eneo la mkutano siku ya tukio kama shahidi muhimu kuthibitisha kuwapo kwa kibali cha mkutano, hakuna kilichopungua katika ushahidi wa Jamhuri.


Alidai kuwa shahidi wa kwanza alieleza mahakamani alivyokuwa akiwasiliana na Dotto ambaye alikuwa eneo la mkutano. Hivyo, hakuna chochote kilichopungua upande wa Jamhuri kwa sababu Dotto alikuwapo eneo la tukio tu.

Naye Nchimbi akiendelea kujibu hoja za rufani, alidai kuwa hakimu alijielekeza kwenye uchambuzi wa makosa hayo yaliyokuwa yanawakabili walalamikaji huku akirejea kesi mbalimbali kwa lengo la kubainisha mambo muhimu yanayotakiwa kuzingatiwa kama washtakiwa wana hatia au la.

Alidai kuwa kama mahakama itapitia hukumu na mwenendo huo ikaona kwamba kazi ya kuchambua hukumu haikufanyika kikamilifu, ikiona upungufu upo basi inayo mamlaka ya kuvaa viatu hivyo vya Mahakama ya Kisutu na kufanya uchambuzi upya.

Alidai kuwa kama mahakama hiyo itaona ulazima wa kufanya upya uchambuzi kwa kuangalia ushahidi huo ni wazi kwamba hatua zote muhimu zimethibitishwa kwa ushahidi uliopo.

Awali, Kibatala alidai kwamba Mahakama ya Kisutu ilikosea kuwapa adhabu Mbowe na wenzake na kuomba Mahakama Kuu itengue hukumu hiyo.



Raia wa Somalia, Jama Ibrahim, akiwa chini ya ulinzi wa askari Polisi, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuhukumiwa kulipa faini ya Sh. milioni moja au kwenda jela miezi 3, kwa kosa la kuishi nchini kinyemela. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Diwani aliyedumu kwa miaka 55 afariki

**Na Ibrahimu Joseph, aliyekuwa MWANGA**

DIWANI wa Kata ya Msangeni, Fihiri Mvungi (80), aliyeongoza kwa nafasi hiyo kwa miaka 55 na kuwa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mwanga mkoani Kilimanjaro kwa miaka 40 amefariki dunia.

Aliingia kwa mara ya kwanza kwenye baraza la madiwani mwaka 1965 akiwa ni kijana wa miaka 25 kabla ya kugawanywa kwa halmashauri ya wilaya ya Same na kupatikana ya Mwanga 1980.

Mvungi aliweka rekodi ya kuwa diwani wa awamu kwa marais wa awamu zote tano kuanzia Mwalimu Nyerere hadi sasa chini ya Rais John Magufuli.

Diwani huyo amekuwa kwenye nafasi hizo kwa muda wote bila kuondoka, tafauti na wanasiasa wengine ambao huongoza kwa kipindi flani na kunyang'anywa nafasi hiyo.

"Unaweza kusema Mvungi alikuwa ni kiongozi pekee aliyechaguliwa na kuhudumu kwenye nafasi hizo mbili kwa muda mrefu kuliko kiongozi yeyote nchini bila kung'atuka wala kuondolewa na wananchi mpaka kifo kilipomchukua," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya Mwanga, Zefrin Lubuva.

Alisema kwa muda mfupi aliofanya kazi na Mvungi, alimfahamu kama kiongozi aliyependa maendeleo na amechangia kwa kiasi kikubwa wilaya hiyo kupiga hatua kwenye mambo mengi kama miundombinu ya barabara.

"Ni kweli tumepoteza kiongozi bora na alistahili kuitwa Baba wa Halmashauri ya Mwanga kutokana na utendaji wake wa muda mrefu, na kutumia busara alizokuwa nazo katika kuongoza vikao vyetu," alisema Lubuva.

Alisema alistahili kuwa kiongozi wa wananchi kwa kipindi hicho chote kutokana na busara na ukaribu aliokuwa nao kwa wananchi wa eneo lake na kufanikiwa kukaa kwa kipindi kirefu.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, Mvungi alipenda maendeleo, mchapa kazi na alitanguliza amani mbele kila ilipotokea kutolelewana kwenye vikao vya baraza la madiwani alisimama katika kutetea jambo pale ilipojitokeza kutoelewana kati ya viongozi na wanasiasa .

Aliongeza kuwa Marehemu Mvungi alimshirikisha miradi ya maendeleoa ya kata yake na mara ya mwisho alikuwa na ujenzi wa ofisi ya Mtaa wa Mamba, ambayo alichangia Sh. milioni 2 mbili, huku Mkurungenzi akichangia Sh. 600,000.

Aidha, alisema kilichokuwa kimebakia ni kuweka umeme na Mvungi alimwambia anatarajia kuwashirikisha wana Mwanga wanaoishi nje ya wilaya hiyo ili wachangie hatua hiyo.

# Uzalishaji wa vazi PPE waongezeka Muhimbili

**Na Mary Geofrey**

UZALISHAJI wa vazi kinga linalovaliwa na watoa huduma wa wagonjwa walioambukizwa Covid-19 umeongezeka kutoka 120 hadi 600 kwa siku sawa na ongezeko la asilimia 400 katika kipindi cha mwezi mmoja.

Uzalishaji huo unafanywa na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), baada ya kuzinduliwa kwa huduma hiyo Aprili 17, mwaka huu na hadi sasa wameshazalisha mavazi 10,553.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma wa MNH, Aminiel Aligaesha, aliyaeleza hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hali ya uzalishaji wa mavazi hayo maarufu kama PPE.

Aligaesha alisema kati ya mavazi waliyozalisha, 5,000 yamesambazwa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) na mengine katika baadhi ya hospitali za rufani za kanda na mikoa, vituo vya afya, taasisi za serikali na hospitali binafsi.

Alisema tayari hospitali hiyo inapokea mahitaji ya mavazi hayo na gharama ya kuuza vazi moja ni Sh. 50,000.

Alisema pia Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imelitambua vazi hilo kupitia barua yenye Kumbukumbu namba BC.248/383/01/13 ya Aprili 23, mwaka huu, hivyo kuiruhusu MNH kuendelea kushona na kufanya usambazaji kote nchini.

Alisema utengenezaji na usambazaji wa vifaa hivyo unazingatia matumizi na uhifadhi unaofuata kanuni za udhibiti wa vifaa tiba nchini, kama walivyoelekezwa na TMDA.



Wafanyakazi wa shamba la miti Sao Hill Mufindi, wakivuna chavua ambazo ni mazao yatokanayo na nyuki katika mizinga inayomilikiwa na shamba hilo, wilayani Mufindi, mkoani Iringa jana. Ujazo wa robo lita ya Chavua, huuzwa kwa 100,000/- hadi 150,000/-. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# ‘Ukila mazao ya nyuki uhakika kuishi miaka mingi’

**Na Francis Godwin, IRINGA**

JAMII imeshauriwa kutumia mazao ya nyuki kwa faida ya kiafya ambayo huwafanya kuishi miaka mingi zaidi na kutozeeka haraka.

Akizungumza na Nipashe jana, katika mahojiano kuelekea kilele cha siku ya nyuki duniani ambacho hufanyika kila mwaka Mei 20, Ofisa Ufugaji Nyuki shamba la miti Sao Hill Mufindi mkoani Iringa, Said Aboubakari, alisema watumiaji wa mazao ya nyuki wanakuwa na uhakika mkubwa wa kuishi kutokana na faida kubwa ya kiafya iliyopo ndani ya mazao ya wadudu hao.

Alisema nyuki anatoa mazao zaidi ya sita na yote yanafaida kubwa kwa binadamu hasa wanaotumia bidhaa zitokanazo na nyuki.

Alisema ufugaji wa nyuki licha ya kusaidia kutunza mazingira, ni muhimu kwa maisha ya binadamu na viumbe hai vyote, kwa kuwa ndio wanaofanya uchavushaji wa mimea.

Alizitaja faida za ufugaji nyuki kuwa ni kupatikana kwa asali na nta, mazao ambayo yana faida kubwa hata katika soko la kimataifa pia dawa ya magonjwa mbalimbali yakiwamo ya kifua, kutibu vidonda vya kuungua na moto, aliyevunjika mguu kuunga mfupa, utunzaji wa vyakula mfano uokaji wa mikate pia viwanda kutengenezea pipi.

Pia, nchi zilizoendelea wanatumia maziwa ya nyuki na utafiti unaonyesha wanaotumia maziwa ya nyuki wanaishi miaka mingi bila kuzeeka haraka.

Ofisa huyo alisema kuwa shughuli za ufugaji nyuki katika shamba hilo zilianza mwaka 2013 na kuongeza mapato ya serikali.

Alisema mbali ya kipato wanachopata bado shughuli hiyo imeongeza ulinzi wa misitu hasa katika utunzaji wa mazingira na kutoa ajira na elimu kwa wananchi kuhusu ufugaji nyuki.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya mji Mafinga, Voster Mgina, alisema kupitia jitihada zao wamewafikishia wananchi elimu ya ufugaji nyuki.

Mhifadhi Mkuu wa shamba la miti Sao Hill Mufindi Juma Mseti, alisema shamba hilo lina umuhimu mkubwa kiuchumi, kijamii na kimazingira kwa taifa kwa kuwa ni kichocheo cha ujenzi wa uchumi wa viwanda kutokana na kuwa na chanzo kikubwa cha malighafi ya viwanda.

Alisema kupitia idara ya ufugaji nyuki, wanaunga mkono jitihada za serikali katika uchumi wa viwanda na wanajipanga kuboresha zaidi na kuona wanaitumia idara hiyo kama kiwanda kikubwa cha uchakataji wa asali bora Tanzania.

# Muswada wapitishwa kusimamia viuatilifu

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

BUNGE limepitisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Afya ya Mimea wa mwaka 2020, ambao pamoja na mambo mengine, umeweka utaratibu wa kusimamia uingizwaji, utengenezaji, usambazaji na matumizi sahihi na salama ya viuatilifu.

Vilevile, unaweka utaratibu wa kutambua, kukusanya na kuteketeza au kurudisha viuatilifu bandia, chakavu na vibebeo vilivyokwishatumika.

Akiwasilisha muswada huo bungeni jana, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alisema muswada huo unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Afya ya Mimea ya mwaka 2020, ili kuunganisha Sheria ya Hifadhi ya Mimea na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu vya Kitropiki.

“Hatua hii itasaidia kuimarisha mfumo utakaosaidia kukabiliana na changamoto mbalimbali zikiwamo za uingizwaji na usambazaji wa viuatilifu bandia,” alisema Hasunga.

Alisema muswada huo utampa mamlaka Msajili wa Viuatilifu kukamilisha baadhi ya majukumu yake kwa mfanyakazi mwingine wa mamlaka baada ya kupata ridhaa ya bodi ya wakurugenzi.

Alisema muswada huo pia utaweka viwango vya adhabu kwa watu watakaokiuka kulingana na uzito wa kosa lililotokea.

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Dk. Christine Ishengoma, akisoma maoni na ushauri wa kamati hiyo, alisema kulingana na sheria inayopendekezwa mtu atakayehitaji kuingiza mimea au mbegu nchini ni lazima kupata kibali kutoka kwa Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu itakayoanzishwa.

“Hata hivyo, kanuni za mbegu nazo zinaelekeza kuwa kibali cha kuingiza mbegu nchini au kusafirisha nje ya nchini kitatolewa na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Kilimo, kuna haja basi kuhakikisha kuwa hakuna mwingiliano wa mamlaka katika utekelezaji wa sheria inayopendekezwa na Sheria ya Mbegu (2003),” alisema Dk. Ishengoma.

Naye Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Kilimo, Paschal Haonga, alisema afya ya mimea inaendana na utafiti, lakini hali halisi ni kuwa kumekuwa na uhaba mkubwa wa fedha katika katika vituo vya utafiti ambalo limekuwa la muda mrefu.

Haonga alisema fedha zao nyingi za utafiti hupatikana kutoka kwa wafadhili.

“Hoja ya msingi ya kujiuliza ni kwa kiasi gani tamko la serikali la asilimia moja ya pato la taifa kupitia Costech zinagawiwa kwa watafiti wa wizara ya kilimo,” alisema Haonga.

Haonga alisema uzalishaji wa mbegu za asili nchini hususani za matunda na mboga umepungua na kwamba mbegu nyingi zinaagizwa kutoka nje.

# Bavicha yatoa neno kauli ya Spika

**Na Elizabeth Zaya**

BARAZA la Vijana la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Bavicha), limemjia juu Spika wa Bunge, Job Ndugai, likisema kwamba kauli za kumkashifu, kumkejeli na kumdhihaki bungeni Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, zinatokana na chuki zake binafsi dhidi ya kiongozi huyo.

Mwenyekiti wa Bavicha Taifa, John Pambalu, alidai kwamba siku za hivi karibuni kumekuwa na tabia ya Spika kumkashifu na kumkejeli mwenyekiti wa chama hicho ambaye ni Mbunge wa Hai na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani bungeni, bila kusahau kwamba ni kiongozi wa chama na ana haki ya kuzungumza na kushauri pale anapoona ana wajibu wa kufanya hivyo.

"Mwenendo wa Ndugai dhidi ya Mbowe ambaye ni kiongozi wa kambi ya upinzani bungeni, kila mtu anautambua, siku hizi Ndugai hawezi kumaliza vikao vya bunge kabla hajamkashifu, kumkebehi na kumdhihaki Mbowe bungeni. Na ukisikiliza hoja za Spika unajiridhisha bila shaka kwamba anachuki binafsi yeye mwenyewe dhidi ya Mbowe," alisema Pambalu.

"Mbowe ni Mwenyekiti wa Chadema Taifa, kwa hiyo anapoona anataka kuzungumza na Watanzania ana haki ya kufanya hivyo, na hakuna sababu ya Spika kutishika na asitumie nguvu kubwa kumkashifu bungeni."

Akizungumzia kuhusu hoja ya wabunge wa Chadema kukatwa sehemu ya mishahara yao kukisaidia chama, Pambalu alisema wanafanya hivyo kwa mujibu wa Katiba na siyo matakwa ya Mbowe.

Alisema Katiba ya Chadema ya Mwaka 2006, toleo la mwaka 2019 kifungu cha 7(a), kinaonyesha namna ambavyo wabunge wa majimbo wanapaswa watoe sehemu ya mishahara yao kusaidia ujenzi wa chama.

Pia, kifungu hicho hicho cha 7(b), kinaeleza namna ambavyo wabunge wa viti maalum wanavyopaswa kutoa sehemu ya mshahara wao kwa ajili ya kukisaidia chama hicho.

"Kwa hiyo wabunge kukatwa sehemu ya mishahara yao kwa ajili ya kukisaidia chama ni matakwa ya Katiba na siyo matakwa ya Mbowe na mambo ambayo yalipitishwa na Kamati Kuu, Baraza Kuu na Mkutano Mkuu wa Chadema Taifa," alisema Pambalu.

Aliongeza: "Kwa hiyo kama hiyo ndiyo sababu ya Ndugai kumchukia Mbowe ni kwa sababu hajui Katiba ya Chadema na sisi kama Bavicha tutampelekea Spika Katiba ya Chadema ili aisome. Spika anamuona Mbowe kama hafai kuwa mbunge, na sisi tunamuona Ndugai kwamba yeye ndiye ambaye hafai kuwa mbunge kwa sababu ukifanya ulinganisho kati ya Jimbo la Hai analoliongoza Mbowe na Jimbo la Kongwa ambalo analiongoza Ndugai, utawahurumia wananchi wa Kongwa."

Pambalu alidai mwenendo wa Ndugai siyo wa kuridhisha kwa sababu kwa nyakati tofauti amekuwa na historia ya kuingia kwenye mgogoro na wabunge pamoja na viongozi mbalimbali hususani wa umma.

"Kwa hiyo Ndugai hatutishi kwa sababu tunamjua na tunafahamu mwenendo wake na namna ambavyo kwa nyakati tofauti amekuwa na migogoro na wabunge mbalimbali pamoja na baadhi ya viongozi wa umma."

"Tunamtumia salamu pia Ndugai kwamba katika uchaguzi wa mwaka huu vijana wengi wa Chadema tumejipanga kuingia bungeni na hata Kongwa tumepanga kulichukua kwa hiyo atafute kazi ya kufanya."



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

**TAMKO LA BEI ELEKEZI ZA KUCHANJIA MIFUGO KWA MAGONJWA YA KIPAUMBELE NCHINI TANZANIA**

Mimi **Prof. Hezron Emmanuel Nonga,** Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo Tanzania, kwa Mamlaka niliyopewa kwa mujibu wa Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya Mwaka 2003 kifungu cha 3(2)(g) na Kanuni za Chanjo na Uchanjaji Na. 180 za Mwaka 2020 Kifungu cha 14(b) na (c) ninatangaza rasmi Bei Elekezi za chanjo za wanyama dhidi ya magonjwa kumi tatu (13) ya kipaumbele ambapo bei ya dukani na ya kuchanjia kwa dozi **HAITAZIDI** viwango vilivyoainishwa kwenye jedwali hapa chini.

Jedwali la bei elekezi kwa chanjo za wanyama dhidi ya magonjwa 13 ya kipaumbele

| Na | Aina ya Chanjo | Bei ya dukani kwa dozi moja (TZS) | Bei ya kuchanjia kwa mfugo (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1 | Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP) | 300 | 550 |
| 2 | Chambavu (Black quarter) | 500 | 800 |
| 3 | Kimeta (Anthrax) | 250 | 500 |
| 4(a) | Mchanganyiko wa Chambavu na Kimeta (TECOBLAX) kwa Ng'ombe | 560 | 800 |
| 4(b) | Mchanganyiko wa Chambavu na Kimeta (TECOBLAX) kwa mbuzi na kondoo | 280 | 500 |
| 5 | Kutupa Mimba (Brucellosis) | 1,000 | 1,500 |
| 6 | Mdondo (Newcastle disease) | 50 | 50 |
| 7 | Mapele Ngozi (Lumpy Skin Disease) kwa ng'ombe | 400 | 600 |
| 8 | Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (PPR) | 200 | 350 |
| 9 | Homa ya mapafu ya mbuzi (CCPP) | 200 | 350 |
| 10 | Ugonjwa wa Miguu na Midomo (FMD) | 2,500 | 3,000 |
| 11 | Kichaa cha Mbwa (Rabies) | 1,000 | 1,500 |
| 12 | Ndigana Kali (ECF) | 10,000 | 17,000 |
| 13 | Homa ya Bonde la Ufa (RVF) | 400 | 700 |

Bei hizi zitatumika kwa Tanzania bara pekee na mabadiliko yoyote ya bei yatatangazwa na Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo kama yalivyojitokeza.

Bei hizi za chanjo dhidi ya magonjwa **13** ya kipaumbele zitaanza kutumika leo tarehe: **13/05/2020**......

Saini: [signature] Tarehe: ......**13/05/2020**..........

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Ondoeni upungufu huu kuhusu corona*

KIASI corona inavyopamba moto, inazidi kuwachanganya watu wengi na ndivyo wanavyohitaji kufahamu zaidi kuhusu maradhi haya kutokana na kuwapo na maelezo mengi yanayohusu ugonjwa huo.

Hii ni kutokana na ukweli kuwa maradhi haya ni mapya na hakuna utafiti wa kutosha kuhusu ugonjwa huo ambao licha ya kusababisha vifo kwa muda mfupi unaleta hofu.

Watu wengi wanakuwa na wakati mgumu kutokana na maelezo mengi yanayotolewa na vyanzo mbalimbali kuhusu dalili za corona, wakieleza kuwa zilizoonekana Italia, China au Marekani sizo zinazojitokeza Afrika.

Kuna maneno kuwa corona ya Afrika haina dalili kama kukohoa, mafua, homa, kukosa pumzi, vichomi na kubanwa mbavu.

Madai ya sasa ni kwamba ugonjwa huo hauna dalili kama hizo badala yake kinachotokea ni mtu anapopata corona huishiwa nguvu, kukosa pumzi, kulegea, kuanguka ghafla na kufa.

Ukweli ni kwamba watu wengi wana taarifa ambazo si sahihi ama ni za kuhofisha kuhusu maradhi hayo na tunachoweza kusema ni kwamba corona ina dalili nyingi na huenda hakuna tofauti na zile zilizoripotiwa Italia, China au Urusi.

Wataalamu wanaeleza kuwa dalili ni nyingi na mojawapo ni kupoteza uwezo wa kutambua harufu na ladha. Pua hushindwa kutambua harufu iwe kali, mbaya au nzuri.

Aidha, ulimi hauwezi kugundua ladha za vitu kama sukari, chumvi, soda, ndimu na mengineyo.

Kuna dalili nyingine kama kupooza mwili mzima kunakotokana na virusi vya COVID- 19 kutengeneza vibonge vya damu vinavyokwamisha damu kusafiri ndani ya mishipa midogo.

Aidha, wataalamu hasa Italia ambao wamefanya utafiti zaidi kwa wagonjwa na hata kuchunguza miili wanaeleza kuwa kuumwa tumbo ghafla, kutapika na kuharisha ni dalili ya corona pia.

Wanaeleza kuwa kuumwa huko kunatokana na mishipa midogo inayosafirisha damu, hewa na chakula kushambuliwa na virusi na kusababisha damu kuganda kutokana na kutengeneza vibonge vidogo vidogo vinavyozuia usafirishaji wa damu tumboni. Yote haya si mapya ni dalili zinazotokea pote duniani.

Suala la kuvaa barakoa nalo lipewa umuhimu kwani inavyoelekea watu hawafahamu sababu za kuzivaa.

Kwa kutumia uzoefu wa mataifa mengine yaliyoathirika hasa China wataalamu wanashauri kuzivaa ili kuzuia maji maji kutoka kwa mtu mwingine akiwamo muathirika zisiwafikie wengine iwapo anaongea, kupiga chafya, miayu na kukohoa.

Barakoa humkinga mtu mwingine na mate au makamasi pamoja na hewa kutoka puani au mdomoni mwa mtu mwingine aliye jirani naye hivyo ni muhimu kuvaa barakoa na si kuzivua wakati unazungumza.

Tunaona kuwa pengine kuna haja ya kutoa elimu zaidi kwa wananchi kuhusu maradhi kuanzia kunawa mikono, kuvaa barakoa, dalili za ugonjwa huu ikiwamo kujibu maswali yanayoulizwa ili kuwapa uelewa wa kutosha.


Kwa hiyo, tunashauri kuwa ni vyema wataalamu wa afya wakatumia vyombo vya habari kuuelimisha umma kuhusu dalili nyingi zinazozungumzwa na kuwashauri hatua za kuchukua ili watu wasiishi kwa hofu bali wawe na uelewa na taarifa sahihi.

Pamoja na vyombo vya habari wataalamu wanaweza kutoa elimu kwenye vituo vya mabasi, kwenye daladala, lakini hata ndani ya magari.

Wanaweza pia kurekodi taarifa hizo na kuziweka kwenye vipaza sauti sehemu mbalimbali wanapofika watu kwenye kuanzia hospitalini, vituo vya polisi, mabasi, makanisani, msikitini, kwenye maduka, vituo vya afya, kwenye saluni na kutumia redio za daladala, za jamii na mabasi ya masafa kutangaza ujumbe huo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Itikadi, mrengo kisiasa visikwamishe kuungana

**WANAWAKE** ni wadau muhimu kwenye demokrasia ya vyama vingi, kwa kuwa washiriki siasa za uchaguzi na ndiyo wapigakura wakubwa na wahamasishaji kwenye kampeni.

Pamoja na hayo, kilio chao cha muda mrefu ni kutopata nafasi za kutosha za uongozi kwenye uchaguzi na hivyo kuonekana kama wamewekwa pembeni kana kwamba hawana uwezo.

Lakini, katika kuhakikisha wanajitokeza kwa wingi kutafuta uongozi, zipo harakati za kuwaunganisha zinazofanywa ili wanapojitokeza, waungwe mkono bila kujali tofauti za itikadi za kisiasa.

Hii inatokana na ukweli kwamba bila kuweka itikadi za kisiasa pembeni na kuungana, hawataweza kufikia kile wanachokusudia cha kutaka usawa katika uongozi huku wenyewe wakiwa si wamoja.

Vinginevyo jamii itaendelea kukumbatia dhana potofu iliyopo kwamba wanawake hawapendani, itaendelea kutawala na hivyo kukwamisha juhudi zao za kutaka kuungana ili kupata nafasi nyingi za uongozi.

Sasa wakati huu ambao nchi inaelekea kwenye uchaguzi mkuu, ni vyema wanawake bila kujali tofauti za itikadi za vyama vyao na kuwa kitu moja ili kuwaunga mkono wenzao watakaojitokeza kuwania uongozi.

Siyo siri wanawake wamekuwa wakitoa kilio kwa kuwa wanatambua mikataba mbalimbali ikiwamo ya kimataifa, ambayo imekuwa ikipitishwa ukiwamo ule wa kuondolewa kwa aina zote za ubaguzi dhidi yao.

Miongoni mwa mikataba hiyo ni ule unaotokana na maazimio ya Mkutano wa Nne wa Kimataifa wa Wanawake uliofanyika Beijing nchini China mwaka 1995, na kuwa chachu kwa wanawake kudai haki zao.

Hivyo ili kuhakikisha wanashika nafasi nyingi za uongozi, ni vyema wakaungana na kuwa kitu kimoja kwenye uchaguzi ujao, kwani wameshajengewa uwezo wa kujiamini na kuvunja vikwazo vinavyowazuia kuwania nafasi za uongozi.

Iwapo watakuwa wamoja kwa kuweka pembeni tofauti zao za itikadi za kisiasa, ushiriki wao wa moja kwa moja kwenye maamuzi ya kisiasa waweza kuendelea kuwa kama ulivyo sasa ingawa wanataka kupiga hatua.

Kwa maana hiyo uchaguzi mkuu wa mwaka huu ni vyema wakawa na umoja ambao utawawezesha kuweka wagombea wa kutosha na kuwapigia kura na hatimaye washinde nafasi za udiwani, ubunge na nyingine.

Binafsi ninaamini kwamba wanawake wana uwezo wa kusimama wenyewe kupata nafasi za uongozi katika siasa kama walivyo wanaume, njia pekee ni kuungana na kujitenga na dhana kwamba hawapendani.

Tanzania ni moja, lakini ya vyama vingi, hivyo wakiona mmojawao awe wa chama tawala au upinzani anakubalika, basi wote hawana budi kumuunga mkono ili aibuke na ushindi.

Ushirikiano huo wa bila kujali itikadi za vyama wanaweza kuzaa matunda ya ushindi, huku wakiendelea kudumisha demokrasia ya vyama vingi vya siasa, kutambua kwamba Tanzania ni moja yenye vyama vingi.

Hiyo ndiyo njia mojawapo ya kupanua wigo wa wanawake wengi zaidi kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika siasa, kuliko kutengana kwa sababu za itikadi za kisiasa.

Siyo wakati tena wa kubaguana kwa itikadi za kisiasa kumuona mwanachama wa CCM, Chadema, CUF kama wanawake wakizingatia hayo, hawatawaona wenzao

wapinzani, anasema mwanzoni mwa mafunzo hayo alikuwa akiwaona wanawake wenzake wa CCM kama maadui, lakini sasa anatambua umuhimu wa kushirikiana bila kujali itikadi za kisiasa.

Sasa ni wakati wa wanawake kuweka ajenda zao mbele kwa ajili ya kufanikisha malengo ambayo wamejiwekea kuliko kuweka itikadi vyama vyao mbele au kukumbatia dhana kuwa wanawake hawapendani.

Vilevile huu si wakati wa kuogopa kujitokeza kuwania uongozi, kwa sababu tayari wameshajengewa uwezo na mbinu mbalimbali za kuwawezesha kufikia pale wanapopakusudia.

Uongozi si kwa ajili ya wanaume tu bali hata wanawake, kwani si kwamba ubebwa kichwani, bali ni mbinu na uwezo wa kuongoza, ambavyo mwanamke na mwanaume wote wamejaliwa kuwa nao.

Uwezo ambao wanawake wamekuwa wakijengewa mara kwa mara, ni muhimu uwe chachu ya kuwaunganisha wanawake kuwa na umoja imara wenye lengo la kufanikisha ajenda yao.

Malalamiko ya muda mrefu ya wanawake ya kukosa haki za msingi ndani ya jamii, ikiwamo kupata nafasi za uongozi katika ngazi mbalimbali yanaweza kumalizika kwa juhudi zao wenyewe kwa kuungana.

HABARI KITAIFA

# DC azuia uporaji mali ya kikongwe

**Na Godfrey Mushi, HAI**

MKUU wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kumtafuta na kumkamata popote aliko mfanyabiashara anayedaiwa kutaka kudhulumu mali na ardhi ya kikongwe Frida Waraskawa, mkazi wa Kijiji cha kwa Sadala wilayani humo.

Waraskawa (83), anayemiliki mali na eneo la ekari tatu katika Mji wa kwa Sadala, anadai kupigiwa simu na mfanyabiashara huyo na kisha kupelekewa notisi ya kuhama katika ardhi yake ndani ya siku 14.

Ole Sabaya alitoa amri ya kukakamtwa mfanyabiashara huyo jana, alipokwenda kukagua eneo hilo na kuzungumza na wakazi wa kwa Sadala.

"Takukuru sikiliza, nilitoa maelekezo kwa Ofisa Tawala amuite na huyo mfanyabiashara akakujibu blabla zake alizokujibu. Sasa ninakuelekeza; Takukuru mtafute popote alipo kwenye mipaka ya Tanzania au nje ya Tanzania, mna njia zenu.

"Mkamateni mniletee mkisaidiana na OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya), halafu sasa nitajua nani mwenye nguvu kati ya serikali na yeye. Na bibi kuanzia sasa mtu yeyote asikutoe hapa na madalali ole wao wasogee kwenye eneo hili. OCD simamia taratibu zote za haki zifuatwe. Wakikukwepa maana yake kuna jambo la ziada wanakukwepa nalo," aliagiza.

Waraskawa anadai kuwa watu asiowafahamu, walimpelekea notisi ya kuhama kwenye eneo hilo, ikielezwa kuwa ni amri ya Mahakama Kuu Kanda ya Moshi.

"Huyu bibi wa miaka 80 alikuwa na haki ya kupata tangu mwaka 1995 na mchakato wake haujabadilishwa hadi leo. Mgogoro ulianza mwaka 2013 hadi leo na huyo mfanyabiashara anasema atabomoa na kujenga super markets kwa siku tatu hapa barabarani.

"Mnapelekana mahakamani na katika hatua za awali bibi huyu alishinda, mwaka 2017 ikatolewa hukumu ambayo bibi hakuwahi kuitwa, ila alileteva barua na madalali kwamba anatakiwa kuondoka.

"Halafu tunyamaze tuwaangalie kwa sababu mna pesa. Hivi matajiri wa Moshi mmekuwaje? Yaani kwa sababu ukiwa na visenti, ukoroge kila mtu? Huyu bibi na uzee huyu mmpeleke wapi kama hamtafuti laana?" Ole Sabaya alihoji.

Katika kutekeleza hilo, kiongozi huyo wa wilaya alisema kibaya zaidi, madalali waliopewa kazi hiyo, hawajawasiliana na uongozi wa aina yoyote.

"Bahati mbaya, hawajatoa taarifa yoyote ya kuja hapa. Siyo kwangu wala hajamweleza OCD wala hawajamweleza Mtendaji wa Kata. Ole wake, nione analeta mtu mguu hapa.

Alimwagiza Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Hai kusimamia agizo lake hilo, huku akionya asitokee dalali yeyote akambughudhi au kugusa mali yoyote ya Waraskawa ambaye ardhi yake amekaa nayo kwa zaidi ya miaka 58.

"Na jambo la pili, bibi huyu alikata rufani mwaka 2017 na ameenda kuulizia, lakini hawakumjibu na nakala ya rufani ninayo hii hapa. Alilipa tarehe 31 mwezi 8 (Agosti) mwaka 2017," alisema.

Ole Sabaya alisema bibi huyo amejikuta akishangaa wanamletea notisi ya kubomoa nyumba yake, akiitaka Idara ya Sheria ya Halmashauri ya Wilaya ya Hai kufuatilia mahakamani kujua hatma yake.

Nipashe imeiona nakala ya notisi hiyo yenye kumbukumbu namba INDE/MS/HC/2020/24 iliyaondikwa Mei 9 mwaka huu kwenda kwa Frida Waraskawa na nakala yake kuelekezwa kwa Msajili wa Mahakama Kuu Kanda ya Moshi.



Wanachama wa kikundi cha kilimo cha umwagiliaji cha 'Sweat no Sweet' cha kijiji cha Bugunda, Kata ya Bwasi, wilayani Musoma, mkoani Mara, wakichukua maji kutoka kwenye mfereji kwa kutumia mashine ya kuvuta maji, ili kumwagilia mazao yao juzi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Jafo aipa TBA mpaka Mei 31 kukamilisha jengo

**Na Julieth Mkireri, CHALINZE**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameagiza Wakala wa Majengo (TBA) wanaojenga Ofisi za Halmashauri ya Chalinze, kukamilisha awamu ya kwanza ifikapo Mei 31 baada ya hapo wasiendelee kwa sehemu iliyobaki.

Alitoa agizo hilo jana baada ya kufanya ukaguzi wa ujenzi wa ofisi hiyo ambao alikiri kutoridhishwa na kasi ya mkandarasi huyo.

"Hakikisheni ifikapo Mei 31, awamu ya kwanza ya ujenzi imekamilika baada ya hapo TBA msiendelee tena na ujenzi na halmashauri mtafute mkandarasi mwingine amalizie eneo lililobaki kwa muda," alisema Jafo. Alisema, haridhiki na namna kazi inavyofanywa na TBA kwa kuwa fedha zipo, lakini kasi ya ujenzi ni ya kusuasua jambo ambalo linachelewesha maendeleo.

"Sio kama nawachukia TBA hapana, kuna maeneo mmefanya vizuri, lakini hapa mmetuangusha sijaridhika na kasi yenu hamfanani na TBA," alisema.

Meneja wa TBA Mkoa wa Pwani, Asha Muyanza, alielezea sababu za kuchelewa kukamilisha mradi huo wa ujenzi kwa wakati kuwa ni pamoja na kupanda kwa gharama za vifaa vya ujenzi na changamoto ya maji.

Mhandisi wa Halmashauri ya Chalinze, John Chizima, alisema jengo hilo la ghorofa tatu hadi kukamilika linatarajia kutumia Sh. bilioni tano na katika awamu ya kwanza Sh. bilioni 1.8 zitatumika.

Mbunge wa Jimbo la Chalinze, Ridhiwani Kikwete, alimpongeza Jafo kwa uamuzi wa kutoa agizo kwa TBA ambao wamekuwa wakichelewesha ofisi hiyo kukamilika kwa wakati.

Akiwa katika Halmashauri ya Kibaha Vijijini, Jafo alitembelea ujenzi wa ofisi ya halmashauri ambao unatarajia kugharimu zaidi ya Sh. bilioni nne na ujenzi wa hospitali ya wilaya ambao alimwagiza mkurugenzi pamoja na watumishi kusimamia kikamilifu miradi ya maendeleo ikamilike kwa wakati na iendane na fedha zilizotengwa.

## Plan International yasaidia Kisarawe vifaa vya corona

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Plan International limekabidhi Wilaya ya Kisarawe, mkoani Pwani msaada wa vifaa mbalimbali vya kukabiliana na janga la virusi vya corona vyenye thamani ya Sh. milioni 76.8.

Msaada huo ulikabidhiwa na Meneja wa Shirika hilo Kisarawe, Marcely Madubi, kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Joketi Mwegelo.

Vifaa hivyo ambavyo idadi yake ipo kwenye mabano ni vipima joto vya mionzi(8), matenki ya maji yenye ujazo wa Lita 500(20), glovu boksi (80),galoni za lita tano za vitakasa mikono (5), vitakasa mikono (210), aproni (80), barakoa FFP2 (30), maboksi ya taulo za kike (100), miwani za kujikinga (30), viatu (120), vifuniko vya mwili (10), mabango (18) na vipeperushi (1500) kwa ajili ya kusambaza elimu.

Akizungumza kwenye hafla hiyo iliyofanyika Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe, Mwegelo alilishukuru shirika hilo kwa msaada walioutoa ambao utasaidia kuimarisha mapambano ya corona.

"Plan International kwa kushirikiana na Shirika la Champion Chanzige (CCO) ambao wametoa msaada wa kutoa elimu kwa njia ya matangazo kwa jamii itakayoambatana na wasanii wa wilaya yetu kundi la Kibajaji, kwa kuzunguka kata 17 alisema.

Alisema utoaji huo wa elimu utakwenda sambamba na ugawaji aa vipeperushi na ubandikaji wa mabango katika ofisi za kata na maeneo mengine muhimu.

Pia alisema Shirika la Plan International litawezesha mafunzo kwa wataalam na viongozi wa ngazi ya wilaya, kata na vijiji wapatao 488.

Kadhalika alisema shirika hilo kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wanaandaa vipindi vitakavyotoa elimu rafiki kwa watoto kupitia runinga na redio.

Naye, Meneja wa shirika hilo, Madubi alisema vifaa vilivyotolewa kwa ajili ya hospitali vina jumla ya thamani ya Sh. milioni 34.2 na Sh. milioni 42.5 zitatumika kwa ajili ya kutoa elimu kwa jamii dhidi ya corona, kukarabati gari la wagonjwa na kuendesha mafunzo wataalam wa afya, walemavu, viongozi wa dini na wa serikali wapatao 488.

Alisema wanaamini vifaa hivyo vitasaidia kuimarisha usalama wa madaktari, wauguzi, wahudumu wa afya na wale wote walio mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya corona.



Mbunge wa Jimbo la Ulanga, mkoani Morogoro, Goodluck Mlinga (mwenye kanzu), akitoa maelezo ya matumizi ya gari la wagonjwa lililotolewa na Rais John Magufuli, kwa ajili ya kusaidia Kituo cha Afya Lupiro, jimboni humo jana. Wengine ni viongozi wa CCM wilayani humo. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# PM asimamisha 3 Temesa tuhuma ubadhirifu mil. 780/-

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amewasimamisha kazi watumishi watatu wa Wakala wa Ufundi na Umeme (Temesa), kwa tuhuma za kuhusika na upotevu wa Sh. milioni 780 zinazotokana na zabuni.

Vile vile, Waziri Mkuu ametoa muda wa miezi miwili kwa taasisi zote za serikali zinazodaiwa na Temesa kiasi cha Sh. bilioni 25.88 ziwe zimeshalipa na iwapo kuna taasisi itashindwa kulipa deni lake hadi Julai 30, 2020 apewe taarifa.

Alitoa maagizo hayo jana alipotembelea karakana ya mitambo ya Temesa, jijini Dodoma na kuwasisitiza watumishi hao wafanye kazi kwa uadilifu na serikali aihitaji wala haitowavumilia watumishi wazembe.

Watumishi waliosimamishwa kazi ni Mkurugenzi wa Huduma Saidizi, Hans Lyimo, Kaimu Mhasibu Mkuu, Jonas Bakuza na Lecian Mgeta, aliyekuwa Mhasibu wa Wakala huo ambaye aliandika barua ya kuacha kazi Aprili 6, 2020.

Ameagiza mtumishi huo arudishwe kazini ili akajibu tuhuma zinazomkabili.

"Kazi hii imefanywa kwa ushirikiano na ofisa wa benki ya CRDB asiyekuwa mwaminifu ambaye naye tutamtafuta hadi tumpate. Fedha hizo zilikuwa kwenye mfumo wa hundi wao wakazibadilisha na kuziweka katika mfumo wa fedha taslimu. Umakini usipokuwapo fedha zote zitakuwa zinaliwa tu."

Kufuatia hali hiyo, Waziri Mkuu amemuonya Mtendaji Mkuu wa Temesa, Japhet Maselle, kutokana na usimamizi wake usioridhisha, amesema mtendaji huyo alikuwa anajua kuhusu upotevu wa fedha katika wakala huo na hakuchukua hatua kwa wahusika.

"...si mzuri kwenye usimamizi unapenda kuacha watu wanaofanya maovu wakiwamo na watumishi hawa watatu. Mtendaji ulikuwa unajua, ulikuwa hauchukui hatua hadi uliposikia nakuja, hii si sahihi sheria zipo na maelekezo ya serikali yapo. Upotevu wa Sh. milioni 780 katika taasisi ni doa."

Waziri Mkuu amesema kufuatia matumizi mabaya ya fedha yanayofanywa Temesa, amemwagiza Mdhibiti na Makaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), akafanye ukaguzi katika wakala huo kutokana na upotevu wa Sh. milioni 780 zilizotakiwa zipelekwe Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Wakati huo huo, Waziri Mkuu amezitaka taasisi zote za serikali zinazodaiwa na wakala huo ziwe zimelipa madeni yote katika kipindi cha miezi miwili ili kuiwezesha Temesa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

"Tukishapata bilioni 25, Temesa hii tukapeleka walau bilioni moja moja kila mkoa watanunua mitambo, watanunua vipuri na magari yatatengenezwa kwa haraka. Magari yote ya serikali lazima yatengenezwe Temesa kwa sababu ya uhakika wa usalama wake."

Pia, Waziri Mkuu ameuagiza uongozi wa wakala huo ufanye maboresho makubwa kiutendaji ikiwa ni pamoja na kufanya marekebisho ya sehemu ya magari kwa kuwa inalalamikiwa zaidi hususani suala la utengenezaji wa magari yanayopelekwa.

Pia, amesema kuwa wakuu wa mikoa, makatibu tawala wa mikoa wanalalamikia gharama kubwa wanazotozwa kwa ajili ya utengenezaji wa magari, hivyo lazima ziangaliwe kama ni halisi.

Kadhalika, ameuagiza uongozi wa wakala huo ujiridhishe kila kivuko kama ni kizima ili kuepusha madhara makubwa yanayoweza kutokea na wavifanyie ukaguzi wa mara kwa mara.

Awali, Mtendaji Mkuu wa Temesa alisema wakala huo unakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwamo madeni makubwa yanayotokana na huduma zao kutolipwa kwa wakati au kutolipwa kabisa.

"...kwa mfano hadi mwezi Machi 2020 tunazidai taasisi za serikali kiasi cha Sh. 25,882,593,038 na wakati huo huo tukidaiwa na wazabuni mbalimbali kiasi cha Sh. 18,959,630,408."

Changamoto nyingine aliyoitaja ni uchakavu wa karakana nyingi zinazomilikiwa na wakala huo katika makao makuu ya mikoa mbalimbali nchini, hivyo kuathiri ufanisi katika matengenezo ya magari ya serikali.

# Uchunguzi kijana anayedaiwa kufia mahabusu sura mpya

**Na Mwandishi Wetu, MOROGORO**

JESHI la Polisi mkoani Morogoro limeanza kufanya uchunguzi kubaini mazingira tatanishi ya kifo cha Kelvin Mapondela (22), ambaye mwili wake bado umehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhia maiti Hospitali ya Mt. Francis, mjini Ifakara kwa takribani wiki tatu kutokana na mvutano baina ya vyombo vya dola na ndugu wa marehemu.

Kelvin alifariki Aprili 28, mwaka huu na ndugu wa marehemu wanadai kifo chake kimetokana na kipigo cha polisi wakati akiwa mahabusu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, akizungumza na waandishi wa habari kutokana na sakata hilo, alisema ofisi yake imefungua jalada na kuanzisha uchunguzi unaoongozwa na Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (RCO) wa mkoa huo.

Mutafungwa, alisema licha ya majibu ya kitabibu kutolewa, ameamua kuongeza nguvu kuwa suala hilo litashughulikiwa na RCO wa mkoa huo kwa kina zaidi.

Alisema, katika uchunguzi huo hawatamwonea mtu yeyote na hata ikibainika kuwa askari wake wamehusika na sheria zitachukua mkondo wake.

Akielezea tukio lilivyotokea, Mutafungwa alisema baada ya kupata malalamiko mengi juu ya tukio hilo, ameamua kwenda mjini Ifakara ili kuonana na ndugu wa marehemu licha ya suala hilo kuwa katika uchunguzi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, alisema Aprili 26, mwaka huu, mjini Ifakara zilipokelewa taarifa kuwa kijana mmoja alikamatwa na vijana wawili kwa tuhuma za kuwaibia waya wa kopa katika ofisi yao ya kununua vyuma chakavu.

Mutafungwa alisema baada ya kutuhumiwa alikamatwa na wenzie na kupelekwa umbali wa kilomita kadhaa na walipofika huko walimshambulia na baadaye kumvua nguo kwa madai ya kutaka kumlawiti.

Alisema siku iliyofuata Aprili 27, kijana aliyeshambuliwa alitoa taarifa katika kituo cha polisi kwa madai ya kushambuliwa na vijana wawili na alipofika nyumbani alikutana na vijana hao wawili akiwamo marehemu kwa nia ya kuomba msamaha kwa kitendo walichokifanya siku ya nyuma.

Wakati wakiendelea kuomba msamaha walishangaa askari mgambo wakiwakamata na kudai wanahitajika polisi kwa makosa waliyoyafanya siku moja nyuma na kuchukuliwa na kupelekwa kituo cha polisi wilaya.

Kamanda Mutafungwa alisema siku iliyofuata ya Aprili 28, vijana wote wawili waliombewa dhamana na walifanikiwa kupata, lakini ilipofika usiku siku hiyo hiyo, walipata taarifa kuwa mmoja kati ya watuhumiwa amefariki dunia.

Alisema katika taarifa ya kifo hicho ndugu wa marehemu walidai kuwa ndugu yao amefariki baada ya kupigwa na polisi wakati akiwa mahabusu.

Kamanda huyo alibainisha kuwa, baada ya kuenea kwa taarifa hizo, Jeshi la Polisi liliamua kufungua jalada la uchunguzi ili kufahamu pale marehemu na mwenzake walipomchukua mtuhumiwa walienda kufanya nini na pia kujua marehemu na mwenzake walipokamatwa kuletwa kituoni walifanywa nini.

Alisema wanachunguza watuhumiwa wote wawili kipi kimewatokea wakati wakiwa mahabusu, huku pia wakichunguza tabia za marehemu na ilikuwaje baada ya kutolewa kwa dhamana.

Kamanda huyo aliwaomba ndugu wa marehemu kama wana ushahidi wowote wapeleke kwa RCO na ataufanyia kazi na kuomba kuuchukua mwili kwa ajili ya mazishi kwa kuwa uchunguzi wa kidaktari umeshafanyika na majibu yamepatikana na kinachosubiriwa sasa ni kubainika wahusika baada ya uchunguzi.

Kwa upande wa ndugu wa marehemu, Steven Marios ambaye amejitambulisha kuwa babu wa marehemu, alidai mjukuu wao aliibiwa waya huo akiwa kazini na siku ya pili walikuja kuchukuliwa na mgambo na kupelekwa kituo cha polisi na siku ya tatu walipoenda kupeleka chai waliambiwa watuhumiwa hao wawili walipigwa sana wakati walipokuwa mahabusu.

Marios, alidai hata baba wa marehemu alipoenda kushughulikia suala la dhamana kwa mwanawe, alidai alipigwa na polisi na walipofanikiwa kumtoa Kelvin alikuwa anashindwa kutembea kutokana na kipigo.

Babu huyo wa marehemu, alidai walimchukua Kelvin na kumpeleka Hospitali ya Mt. Francis na alipofika alikimbizwa chumba cha uangalizi maalum (ICU), baada ya hali yake kuwa mbaya na ilipofika usiku alifariki dunia wakati akihangaikiwa kuongezewa damu.

Ndugu mwingine wa marehemu, aliyejitambulisha jina la Focus Mapondela, alidai kinachowashangaza ndugu yao alikuwa mzima wa afya wakati anakamatwa, lakini alipotoka mahabusu alikuwa katika hali mbaya.

Mapondela, alisema wamepokea ushauri wa kamanda huyo wa polisi kwa kumleta Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa wana imani haki itatendeka na suala la kumzika marehemu watakaa kama familia kisha kutoa majibu na kutangaza siku ya maziko.

## HABARI KITAIFA

## Wateja Tigo Pesa wavuna bilioni 2.7/-

**Na Mwandishi Wetu**

SHILINGI bilioni 2.7 zimetolewa na Kampuni ya Tigo Tanzania katika robo ya kwanza ya mwaka 2020 kwa wateja wake ambao wanatumia huduma ya Tigo Pesa.

Fedha hizo ambazo wateja wa Tigo wamepata ni mwendeleo wa kampuni hiyo kugawana faida na wateja wake ambapo huo ni mgao wa 24 tangu kuanza utaratibu huo.

Akizungumzia utaratibu huo wa kugawana faida na wateja, Kaimu Ofisa Mkuu wa Huduma za Fedha Tigo Tanzania (MFS), Angelica Pesha, alisema kampuni hiyo hadi sasa imetoa Sh. bilioni 100.9 tangu waanzishe utaratibu huo Julai 2014.

Pesha alisema katika robo ya kwanza ya mwaka huu kutokana na janga la ugonjwa wa COVID-19 unaosababishwa na virusi vya corona ambapo biashara zimeshuka kutokana na mzunguko wa kifedha kuwa mgumu, gawio hilo kwa wateja litawasaidia sana.

"Kutokana na janga la COVID-19, limeathiri nchi na wananchi duniani kote na hapa Tanzania, faida hii tunawapa watumiaji mmoja mmoja, watoa huduma za rejareja na wajumla na wadau wengine wa Tigo," alisema Pesha.

"Tunajisikia faraja kutangaza ongezeko la faida kwa mara ya 24 mfululizo ambayo inatoa nafuu kwa wateja wa Tigo Pesa, hivyo kuwasaidia katika kupata huduma za kijamii kwani wamekuwa watu muhimu katika kutuwezesha kutimiza malengo yetu," aliongeza.

Kaimu Mkuu huyo alisema huduma hiyo imesababisha kutimiza majukumu yao hasa katika huduma ya fedha kwa wateja wao.

Pesha alisema Tigo inaendelea kuongeza faida kwa kuongeza wateja wa Tigo Pesa ili kuchochea ongezeko la faida kibiashara.

Alisema hadi sasa Tigo Pesa ina mtandao wa wafanyabiashara zaidi ya 50,000 nchini kote na wakala zaidi ya 110,000 wanaosaidia mahitaji ya wateja ya kila siku.

**"Tunajisikia faraja kutangaza ongezeko la faida kwa mara ya 24 mfululizo inatoa nafuu kwa wateja wa Tigo Pesa, hivyo kuwasaidia katika kupata huduma za kijamii kwani wamekuwa watu muhimu katika kutuwezesha kutimiza malengo yetu," aliongeza.**

# Madereva wapewa masharti matumizi magari ya wagonjwa

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

MKUU wa Wilaya ya Morogoro, Rejina Chonjo, amewaonya madereva wa magari ya kubeba wagonjwa, kuacha mara moja tabia ya kuyatumia kwa ajili ya shughuli binafsi ikiwamo kubebea mikaa.

Badala yake mkuu huyo wa wilaya alisema yatumike kama yalivyokusudiwa.

Chonjo alitoa onyo hilo baada ya kupokea gari la wagonjwa lililotolewa na Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood, lenye thamani ya Sh. milioni 42 kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Sabasaba Manispaa ya Morogoro.

"Zipo taarifa za baadhi ya madereva kuyatumia magari hayo ya kubebea wagonjwa kwa ajili ya kubeba mikaa na vitendo vya uhalifu kwa kuwa yanaweza kupita popote yakiwasha king'ora, unaweza kusikia hili gari limekamatwa Ulanga limebeba bangi," alionya.

Aidha, aliwataka wahudumu wa afya kwa kushirikiana na dereva wa gari hilo kuhakikisha wanalitunza na kulitumia katika matumizi yaliokusudiwa na kuwataka wananchi kutoa taarifa wanapoona linatumika vibaya.

Alimpongeza Mbunge Abood kwa juhudi anazofanya.

Mganga mfawidhi wa kituo hicho, Dk. Vulfrida Kyala, alisema uwapo wa gari hilo katika kituo hicho kutasaidia kupunguza vifo vya wajawazito pale wanapohitajika kuhamishiwa katika Hospitali ya Rufani. Alisema katika kituo hicho kuna wodi ya wajawazito Agosti 2019, ikiwa na uwezo wa kuhudumia wajawazito 18 kwa wakati mmoja na imelenga kuhudumia 2,585 wa kata hiyo.

Alisema hadi sasa kinamama waliojifungulia hapo ni 835, huku 217 wakipewa rufani kwenda hospitali ya mkoa kabla ya kujifungua kwa ajili ya huduma zaidi.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Sheila Lukuba, alisema uongozi wa manispaa utahakikisha gari hilo linatumika kwa matumizi sahihi sambamba na kulitunza.



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (kulia), akiwasha umeme katika nyumba ya mkazi wa Kijiji cha Bugwego, Kata ya Bwongera, wilayani Chato, mkoani Geita juzi, alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji umeme vijijini katika maeneo hayo. **PICHA: ZUENA MSUYA**

# DC asuka mkakati kuzuia mimba za wanafunzi likizo ya corona

**Na Yasmin Protece, MKURANGA**

MKUU wa Wilaya ya Mkuranga Mkoa wa Pwani, Philberto Sanga, ameagiza watendaji wa kata zote zilizopo katika wilaya hiyo kwenda kutoa elimu ya afya ya uzazi kwa wazazi na walezi wa wanafunzi.

Wanafunzi hao ni wa shule za msingi na sekondari kwa lengo la kuwaepusha na mimba zisizotarajiwa hasa kipindi hiki cha mapumziko kama tahadhari ya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona.

Sanga aliyasema wakati wa uwasilishwaji wa taarifa za kata za robo ya tatu kwa mwaka wa fedha 2019/2020, na kusisitiza kuwa anasikitishwa na baadhi ya wazazi wanaowaachia watoto wa shule kufanya biashara ndogo na wengine kuzurura mitaani.

Badala yake aliwataka wakae nyumbani wakijisomea, hatua itakayowasaidia kujiepusha na vitendo vinavyoweza kuwaathiri kielimu baada ya shule kufunguliwa.

Baadhi ya madiwani waliunga mkono agizo hilo na kusisitiza ya kuwa wazazi wawe makini na watoto wao ili kuepusha kuchukuliwa hatua za kinidhamu na hatimaye adhabu za vifungo au faini kwa wale wote watakaoenda kinyume cha sheria za malezi ya watoto wadogo na wanafunzi.

Pamoja na kupokea agizo hilo, baadhi ya madiwani walimpongeza Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi na Mbunge wa Jimbo la Mkuranga, Abdallah Ulega, kwa juhudi anazozifanya katika kuwaletea wananchi wa Wilaya ya Mkuranga maendeleo katika sekta za elimu, afya na miundombinu ya barabara.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Mhandisi Mshamu Munde, aliwashukuru wakuu wa idara na vitengo kwa juhudi wanazozifanya za kusimamia miradi ya maendeleo na kuwataka kusimamia ubora na viwango vya hali ya juu miradi yote inayoanzishwa katika wilaya ili iwe na hadhi kwa jamii na maendeleo ya wilaya kwa ujumla.

## Mgogoro Hifadhi Ruaha, wakazi Mbarali kutatuliwa

BUNGE limeelezwa kuwa serikali ipo katika hatua za mwisho za utatuzi wa mgogoro wa mpaka kati ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na wakazi wa baadhi ya kata za Wilaya ya Mbarali.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Wizara ya Maliasili na Utalii ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Sophia Mwakagenda.

Katika swali la mbunge huyo, alihoji ni lini serikali itatatua mgogoro kati ya hifadhi hiyo na wananchi wa Kata za Madibira, Miyombweni, Igawa, Rujewa, Songwe, Mapogoro na Ruhanga kupitia Tangazo la Serikali (GN) 28 Mbarali ili kuwaondolea hofu wananchi.

Alisema wakulima na wafugaji wamekuwa wakikamatwa kila siku na kudhaniwa kuwa wanaendesha shughuli zao sehemu ya hifadhi.

"Je, ni kwa nini wananchi ambao ni wakulima na wafugaji wanaendelea kukamatwa kwa amri ya Mkuu wa Wilaya?" Alihoji.

Alieleza kuwa wakati Waziri Mkuu akiahirisha Bunge la Bajeti 2016/17 alitoa kauli kuwa wananchi wasibughudhiwe mpaka pale timu ya wataalamu itakapokuwa imerejesha taarifa ya utafiti wa mgogoro huo ndipo serikali itatoa tamko la mwisho kuhusu mgogoro huo.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema serikali ipo katika hatua za mwisho za utatuzi wa mgogoro huo.

"Ikumbukwe kuwa baada ya agizo la Rais John Magufuli, la kumaliza kero za ardhi katika maeneo yaliyohifadhiwa, timu ya mawaziri wa wizara za kisekta, iliundwa kushughulikia migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini ikiwamo Wilaya ya Mbarali kati ya wakulima, wafugaji na hifadhi hiyo," ilisema.

Ilieleza kuwa taarifa na mapendekezo ya timu hiyo yaliwasilishwa kwenye mamlaka husika kwa ajili ya kutoa maamuzi.

"Maamuzi hayo yalitolewa taarifa na Waziri Mkuu mwezi Septemba 2019 kuwa jumla ya vijiji 920 kati ya 975 vilivyokuwa na migogoro na maeneo yaliyohifadhiwa nchini vitabakia kama vilivyo," ilisema.

Ilibainisha kuwa vijiji hivyo vinajumuisha pia vijiji katika kata hizo vyenye mgogoro wa GN namba 28 ya 2008.

Aidha, ilisema wizara kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (Tanapa) pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Mbarali wanaendelea kutekeleza maagizo ya Waziri Mkuu kulingana na kauli aliyotoa kuwa wananchi wasibughudhiwe hadi timu ya wataalamu itakapokuwa imerejesha taarifa ya utafiti wa mgogoro huo.

Hata hivyo, ilisema kuna baadhi ya wananchi ambao wameendelea kufanya shughuli za kibinadamu hifadhini kama vile kufungua mashamba mapya, kuanzisha makazi na kuchunga mifugo katika maeneo ambayo hayana mgogoro au yale ambayo wananchi walikwisha kulipwa fidia na kuhamishwa.

# Mafunzo ya uandaaji vyakula vya virutubisho rasmi mikoa 6

**Na Augusta Njoji, DODOMA**



WIZARA ya Kilimo imeanza kutoa mafunzo ya uzalishaji, utayarishaji na ulaji wa vyakula vilivyoongezewa virutubisho katika mikoa sita.

Mikoa hiyo ni yenye zaidi ya asilimia 40 ya watoto wenye udumavu, ambao ni chini ya miaka mitano.

Mikoa hiyo ni Njombe (53.6%), Rukwa (47.9%), Iringa (47.1%), Songwe (43.3%), Kigoma (42.3%) na Ruvuma (41.0%).

Hayo yalibainishwa jana bungeni na wizara hiyo ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Mkinga (CCM), Dunstan Kitandula (pichani).

Katika swali lake, mbunge huyo alisema utapiamlo katika nchi ni janga kubwa kwa sababu kila watoto 100, watoto 30 wana tatizo la udumavu wa akili.

Pia, alisema kila watoto 100, watoto 59 wenye umri kati ya miezi 6 na miaka 5 wana upungufu wa damu, kutokana na hali hiyo, inagharimu serikali asilimia 2 ya pato la Taifa sawa na dola za Marekani milioni 518 kuhudumia dawa za vitamini 'A' na folic acid.

"Je, kwa nini serikali isiwekeze katika upatikanaji wa mbinu bora za kilimo ili kuinua kiwango cha upatikanaji wa lishe bora ya kudumu kama njia ya kukabiliana na tatizo hilo?" Alihoji.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema mpaka sasa mafunzo hayo yameshafanyika

katika Mkoa wa Iringa, ambayo yalihusisha wanawake walio katika umri wa kuzaa, wanaume, viongozi na wataalamu katika ngazi ya kata na halmashauri.

Aidha, ilisema katika mafunzo hayo mashamba darasa 12 yalianzishwa katika kata 8 kwa lengo la kufanyia mafunzo kwa vitendo.

"Mafunzo haya yanalenga kujengea uwezo wa jamii katika kuzalisha na kutumia mazao yaliyoongezewa virutubishi kibaiolojia hatimaye kukabiliana na upungufu wa vitamini na madini mwilini hususan watoto chini ya miaka mitano na kinamama wajawazito na wanaonyonyesha," ilisema.

Wizara ilisema ni miongoni mwa wizara 8 zinazotekeleza masuala ya lishe hapa nchini.

"Katika kutekeleza Mpango Jumuishi wa Kitaifa wa Lishe, Wizara ya Kilimo inalo jukumu la kuhakikisha kuwa mazao yenye virutubisho kwa wingi yanazalishwa na kutumiwa ipasavyo," ilisema.

Kadhalika, ilisema kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, virutubishi vinaongezwa katika baadhi ya bidhaa zenye matumizi makubwa.

"Kwa mfano, madini chuma, zinki na vitamini 'B' huongezwa kwenye unga, ambapo vitamini 'A' huongezwa katika mafuta ya kupikia," ilisema.

Ilieleza wizara pia ina jukumu la kuelimisha jamii kuhusu uzalishaji wa mazao mchanganyiko na matumizi ya vyakula vinavyotokana na mazao hayo.

"Vituo vya utafiti wa mazao ya kilimo nchini vikishirikiana na wadau vimekuwa vikizalisha aina mbalimbali za mbegu za mazao yaliyoongezewa virutubisho kibaiolojia mazao hayo ni pamoja na viazi lishe, mahindi yenye vitamini 'A' kwa wingi, pia maharage yenye madini chuma na zinki kwa wingi," ilisema.

Hata hivyo, ilisema mazao hayo yameanza kuzalishwa na kutumiwa sehemu mbalimbali nchini, mfano viazi lishe vinazalishwa mikoa ya Morogoro, Pwani, Iringa, Singida, Shinyanga, Mwanza na Kagera.

"Katika kuhakikisha usimamizi mzuri wa mazao haya, wizara imeandaa mwongozo wa mazao yaliyoongezewa virutubishi kibaiolojia ambao utatumiwa na wadau wote katika mnyororo wa thamani wa mazao haya," ilisema.

# Mbunge ahoji takwimu ajali za barabarani kutofautiana



MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Fatma Toufiq (pichani), amehoji kuwapo kwa utofauti wa takwimu za ajali nchini zinazotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO) na Jeshi la Polisi.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo alisema kwa mujibu wa takwimu za WHO, takribani Watanzania 16,000 hupoteza maisha kwa mwaka kwa ajali za barabarani.

"Hata hivyo takwimu za Jeshi la Polisi zinaonyesha ni watu 300 hadi 4,000 wamepoteza maisha kwa mwaka kwa ajali. Je, ukweli upo wapi katika upatikanaji wa takwimu?" Alihoji.

Katika majibu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ilisema takwimu sahihi za ajali, vifo na majeruhi ni zinazotolewa na Jeshi la Polisi.


"Huripotiwa katika vituo vya polisi na hukusanywa na askari polisi wa usalama barabarani ambapo takwimu hizo hutolewa na kutumiwa pia na Idara ya Takwimu ya Taifa katika kuandaa taarifa ya nchi inayohusiana na masuala ya ajali," ilisema.

Aidha, ilisema kwa kuzingatia sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 iliyorejelewa mwaka 2002 na marekebisho yake ya mara kwa mara, Inspekta Jenerali wa Polisi anao wajibu wa kukusanya na kutoa takwimu za taarifa za usalama barabarani kwa umma.

Hata hivyo, ilisema takwimu zinazotolewa na WHO ni takwimu za makisio na katika takwimu zao kwa taarifa ya mwaka 2018 inaonyesha ajali za barabarani zilisababisha vifo 3,256 takwimu ambazo ni sahihi kwa kuwa chanzo chake ni jeshi hilo.

Kutokana na hilo, wizara ilisema kwa takwimu za takribani Watanzania 16,000 hupoteza maisha kwa mwaka hazina ukweli wowote.

## Hatua kujiangalia Rais Uhuru, Ruto kukwepa Kenya ya 2007



Ukurasa 14



Ukurasa 12

## Uwezo, maajabu walinzi 12 wa Rais Kim Jong-un-2

siasa
JUMATANO MEI 20, 2020
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

BALOZI MAHIGA

# Mbobezi wa UDSM aliyetumika UN kuleta amani maeneo korofi

**Na Ani Jozeni**

TUNAPOENDELEA kukumbuka maisha ya tunu Balozi Dk Augustine Mahiga, aliyeondoka akiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, pamoja na hilo ana sifa lukuki. Mojawapo ni kuzama na kutekeleza kwa vitendo nadharia za uhusiano wa kimataifa alizowahi kujifunza na kufundisha katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam -UDSM.

Ni wazi kuwa licha ya kuwapo maelezo na mchango wake kitaifa na kimataifa, Balozi Mahiga, bado kuna nafasi ya kutafakari maisha yake na nini aliwakilisha katika diplomasia na maeneo mengine ya maendeleo.

Hakuna wanadiplomasia wawili wanaofanana, au wakuu wa idara za Umoja wa Mataifa kutoka Tanzania wanaoweza kufanana. Kila mmoja anakuja na mchango wake na mwelekeo wake, unaofafanua alichokifanya na alama anazoziacha.

Kazi ya Dk. Mahiga katika miaka takriban 42 tangu aondoke Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1978 akiwa mhadhiri wa Taaluma ya Siasa na Utawala, ni ya aina yake.

Ni mmoja kati ya wasomi wa Chuo Kikuu UDSM walioondoka katika umri mdogo na kuingia anga tofauti za utumishi wa kimataifa.

Kwa sehemu kubwa ya uteuzi wa aina hiyo kwa upande wa wahadhiri chuoni hapo, mara nyingi zaidi mtaalamu husika anakuwa nje kwa muda halafu anaendelea na kazi chuoni.

Kuna kundi lingine la wasomi ambao wanateuliwa katika kazi za kitaifa na wasirudi tena chuoni, lakini mandhari yao ya kikazi kimsingi yanakuwa hapa nchini, kwa mfano kwa uteuzi wa kusimamia mashirika ya umma au wizara iwe ni ukatibu mkuu au uwaziri.





Balozi Mahiga (kushoto) akiwa na aliyekuwa Katibu Mkuu wa UN, Ban Ki-moon (mwenye kizibao), kwenye shughuli za umoja huo. **PICHA: MTANDAO**

Wapo waliotoka katika ngazi kama hiyo na kurudi kwa muda mfupi halafu kuendelea na kazi za kitaifa, akiwamo Profesa Mark Mwandosya, mhandisi umeme aliyepata sifa lukuki katika masomo yake.

Akiwa amefikia ngazi ya ukatibu mkuu alirudi chuoni kufundisha, baadaye akawa mbunge na kuendelea na uwaziri na ukawa ndiyo mwisho kuwepo chuoni hapo.

Dk. Mahiga alikabidhiwa kazi zinazoendana na taaluma yake ya udadisi na uchambuzi wa kisiasa, aliyoianza akiwa mshauri Ikulu kabla ya kukabidhiwa makabrasha tofauti katika taasisi nyeti na punde akaonekana anaweza kujenga hoja na kuwezesha inachoamini Tanzania kieleweke, hivyo akawa ndiye mtu anayefaa kuchukua nafasi ya Dk. Salim Ahmed Salim kama balozi Umoja wa Mataifa.

Ni viatu ambavyo ingekuwa vigumu kwa mtu yeyote kuvivaa, na haikuwa jambo la kushangaza kuwa hapakuwa na 'bashasha' kama za Dk. Salim wakati wake, kwani mwanadiplomasia huyo alikonga nyoyo za dunia kwa suala la China.

Dk. Mahiga alikuwa katika kile Waingereza wanaita 'eye of the storm,' jicho la tufani, kwa muda wake wote wa utumishi serikalini na kama mtumishi wa kimataifa, kwa uteuzi wa makatibu wakuu tofauti wa Umoja wa Mataifa.

Kwa kuwa hakuwahi kusahaulika katika ngazi yoyote aliyofikia, akapewa jukumu moja baada ya jingine, yaani kutoka chuoni kuingia Ikulu, Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa, kuchukua nafasi ya Dk. Salim, halafu UN kumchukua na kubaki naye muongo mzima, si kazi rahisi.

Ni mtu aliyeaminika katika maeneo nyeti, na ni wazi alileta tija kuongea na watu wasioelewa diplomasia, katika vituo vigumu vya kazi kama Liberia na Somalia.

Kusema kweli, kazi hizo za upatanishi wakati wa vita zinahitaji mtu mtulivu ambaye yuko tayari kuhatarisha hata maisha yake ili kuokoa wengine endapo kwa juhudi zake urefu wa vita unaweza kupungua, au mifumo ya amani ikaharakishwa.

Kwa maana hiyo, hayati Dk. Mahiga ameitendea haki taaluma ya uelewa wa mifumo ya kiusalama katika maisha ya nchi na mazingira tofauti ya kimataifa, kuliko mwanadiplomasia mwingine ambaye nchi hii imewahi kuwa naye.

Hakuwa mtu aliyepewa tu kazi ya ubalozi ila alianza katika ushauri, na baada ya miaka 10 akiiwakilisha nchi, akawa sasa mshauri wa kimataifa. Alikuwa anabadilishiwa vituo vya kazi na siyo kupanda ngazi au kupata sifa.

Kwa maana hiyo haitakuwa sahihi kumlinganisha Dk. Mahiga na baadhi ya wale waliopewa nafasi kubwa UN kwani zaidi walikwenda kama watawala.

Hawakuingizwa katika maeneo ya misukosuko na vita yanayohitaji mtaalamu wa amani, kujenga hoja kwa taabu mbele ya watu wanaongoja kikao hicho kiishe waendelee na mipango yao ya mashambulizi.

Balozi Mahiga siyo tu alifanya kazi hiyo na 'Simba wa Liberia' halafu miongoni mwa wapiganaji 'vita isiyoisha' nchini Somalia na akawa anapata usinginzi anajiandaa kuketi mezani na watu hao hao kwa miaka kadhaa na UN ikawa tegemezi kwake hadi amefikia umri unaokaribia miaka 70 haikuwa mazingira ya kawaida.

Kimsingi ni kuwa Mahiga amethibitisha kuwa 'taaluma ya siasa' au ya amani' ni kitu gani, ila kuna ziada ambayo inabidi iandane na busara na hata imani.

Ni hali ambayo alikuwa anapewa kazi ambazo si wengi walikuwa wanazitaka na kwa hakika siyo wengi walikuwa wanaziweza, wadumu hapo na hata kufurahia kutoa mchango angalau kidogo kufikia amani. Hawakuwa wengi.



Rais Kim Jong-un (katikati ya walinzi), akiwa ndani ya ngome ya makomandoo. Ulinzi wake unaelezwa kuwa ni wa kipekee duniani. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

# Uwezo, maajabu walinzi 12 wa Rais Kim Jong-un-2

**Na Joseph Muhozi**

Ni ukweli kuwa, ni vigumu kwa mwanga wa mshumaa kudumu katikati ya upepo wa kimbunga, vivyo hivyo haiwzekani kwa inzi mwenye nia ovu kumsogelea kiongozi wa Korea Kaskazini, Kim Jong-un, kutokana na ulinzi madhubuti unaomzunguka.

Huyu ni Rais ambaye analindwa kikamilifu. Japo kiumri ni mdogo lakini anasifika kutengeneza makombora hatari ya nyuklia yanayodaiwa kutishia usalama wa dunia. Madai yanayotolewa na Marekani. Wiki iliyopita tulieleza namna anavyolindwa na makondoo wenye weledi wa hali ya juu wakiwamo wanaokimbia kulizunguka gari lake. Aidha yapo mengine mengi na sasa tunamalizia sehemu ya mwili ya ulizi huo wa kikomandoo duniani.

**NI ULINZI KILA KITU**

Teknolojia ya nasaba (DNA) ni kama silaha siku hizi maana utaalamu huo ukidaka chochote kinachotoka kwenye mwili wa binadamu unaweza kukitumia kueleza mengi yanayokuhusu. Kwa hiyo lengo la GC ni kuzuia ili watu wasipate hata unywele mmoja ulioanguka wa Kim Jong-un, Ndiyo maana kuna watu wako kazini kuulinda muda wote.

Kikosi hiki cha the 'GC' au Guard Commando. Huhakikisha usalama wa eneo la ofisi yake, nyumbani kwake au sehemu yote anayotembelea iwe ni ndani au

> Kim ameliongoza taifa hilo kuwa na silaha za hatari na ulinzi wa ajabu. Ni nchi ndogo ambayo idadi ya watu wake ni takribani nusu ya idadi ya wananchi wa Tanzania.



Rais Kim Jong-un.

nje ya nchi hiyo.

Kikosi hiki pia huundwa na makomando ambao wamepitia mtindo uleule wa kufuatiliwa, kufanyiwa tathmini, kuhakikiwa na hatimaye kupitia mafunzo makali ya kimwili, kisaikolojia na kitaalam kama wale makomando wa 'The Main Office of Adjutants'.

Mfano mwingine ni wale waliofuatilia safari ya Kim Jong-un nchini Singapore, zilishuka ndege tatu kutoka Pyongyang, mji mkuu wa Korea Kaskazini kumsindikiza kiongozi wao, mbili kati ya hizo zilikuwa zimewabeba maofisa wa kikosi cha ulinzi kutoka 'CG'.

Kikosi hiki chenye wanaume na wanawake, ndiyo waliohakikisha usalama wa simu aliyokuwa akitumia Kim Jong-un na kumpa msaada wa ulinzi wa kimtandao kwenye kompyuta yake.

Waliweka ulinzi mkali katika eneo la Hoteli ya St. Regis, ambapo Kim Jong-un alifikia.

Kadhalika, walihakikisha kila alichokula, kuvuta au kunywa nchini Singapore wanakipima kwanza kujiridhisha na usalama. Kikosi hiki pia kilikuwa na madaktari wawili wabobezi, mbali na madaktari wake.

Kwa ujumla, makomando kutoka kikosi cha GC, hutengeneza mzunguko wa pili baada ya makomando wale 12 wanaomlinda, ingawa mzunguko huu huwa hauonekani kwa uharaka.

Pia, wakiwa nchini Korea Kaskazini huunda mzunguko wa tatu ambao unakuwa karibu na watu wanaojipanga katika maeneo anayopita kiongozi huyo.

Kwahiyo, wakati wale walinzi 12 wanaokimbia kuzunguka gari alilopo Kim Jong-un wakiwa kivutio cha macho ya wengi na taswira ya ulinzi wa kiongozi huyo, nyuma ya pazia huwa kuna mizunguko mingine miwili ya ziada isiyoonekana dhahiri ambayo ni huweka ulinzi mkali zaidi kuhakikisha hakuna hata 'inzi' mwenye nia ovu anayesogea karibu na kiongozi huyo.

Hii ni sehemu ndogo ya ulinzi binafsi wa Kim Jong-un, kiongozi mwenye umri mdogo unaosadikika kuwa ni kati ya miaka 36 na 37. Ingawa ukisoma kwenye wikipedia wameamua iwe 36 kwa maana kuwa amezaliwa mwaka 1984.

Moja kati ya vitu adimu zaidi kupata nchini humo ni taarifa kuhusu Kim Jong-un na serikali yake, hiyo ni siri kuu hadi wao wenyewe waamue kukupatia. Wananchi wanaishi kizalendo kutokana na jinsi walivyofunzwa kuanzia utotoni kumheshimu kiongozi wa nchi hiyo na serikali.

Ni nchi ya Kikomunisti. Sauti ya Kim ni sauti ya kiongozi na huheshimiwa kama amri inayopaswa kufanyiwa kazi ipasavyo. Na karibu kila kijana hupewa mafunzo angalau ya msingi ya kijeshi.

Kwa makala kadhaa zinazozungumzia maisha ya Wakorea nilizowahi kuziona, wananchi wa Korea Kaskazini wanaishi maisha bora kuliko baadhi ya wananchi wa nchi kadhaa za Bara la Asia. Ingawa kinachosimuliwa sana mitandaoni kinaogofya kuhusu nchi hii, haina maana kuwa ndani ya Korea Kaskazini watu hawatabasamu. Kama ilivyo kwa nchi nyingi, wapo wanaotabasamu na wapo wanaolia.

Rais Donald Trump wa Marekani ambaye awali aliwahi kukaririwa akimuita Kim Jong-un kuwa ni 'mwehu' na kumpa majina ya dharau kama 'mtu mdogo anayemiliki makombora', baada ya kukutana naye na kufanya mazungumzo alibadili mawazo.

Trump anasema amegundua Kim ana akili kubwa, anajua kufanya makubaliano kwa ajili ya nchi yake. Pia, Trump anaona kama Korea Kaskazini inaweza kuwa kati ya nchi zenye uchumi mkubwa duniani endapo itaondolewa vikwazo.

Kim ameliongoza taifa hilo kuwa na silaha za hatari na ulinzi wa ajabu. Ni nchi ndogo ambayo idadi ya watu wake ni takribani nusu ya idadi ya wananchi wa Tanzania. Uhusiano wake imara na China na washirika wake pia ni moja kati ya mambo yanayowapa nguvu zaidi wana Korea ya Kaskazini.

UCHAMBUZI

# Baada ya tathmini ya miaka 20, NCCR kurudi ulingoni kivingine?

**Na Sabato Kasika**



Waliokuwa viongozi wa chama hicho wakiwa katika kikao enzi hizo kilipokuwa na nguvu. Kulia ni Augustine Mrema, Mabere Marando, Ndimara Tegambwage na James Mbatia. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

CHAMA cha NCCR- Mageuzi, kinajinasibu kuwa kinaelekea kurudi kwenye nafasi yake ya chama kikuu cha upinzani nchini, kama ilivyokuwa baada ya uchaguzi mkuu wa kwanza ndani ya mfumo vwa vyama vingi uliofanyika mwaka 1995.

"Tumetembea nchi mzima na kwa bahati waasisi wa chama waliojitoa sasa wanarudi ndani ya chama," anasema Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi, James Mbatia.

Mbatia anakumbusha kuwa chama hicho ndicho kilichoasisi mageuzi ya siasa za vyama vingi nchini, lakini kutokana na uchanga wa mageuzi na viongozi wake kikapata msukosuko mwaka 1995.

Anasema, msukosuko huo ulisababisha chama kudhoofika kisiasa na kugawanyika makundi mawili yaliyowaachia hasara, lakini sasa wamefanya tathmini na wanarudi upya.

"Tumefanya utafiti wa masuala ya kisiasa, uongozi na demokrasia, tumepata majibu yanayotokana na maswali magumu waliyonayo Watanzania, hivyo wananchi sasa wameanza kutuelewa, wanajiunga na chama chetu," anasema.

Mwenyekiti huyo anafafanua kuwa, utafiti huo wa kina ulioanza tangu mwaka 2000, kwa kutambua kuwa walikuwa na viti vingi wakavipoteza na sasa wamejiandaa kushinda. "Tuna matumaini ya kushika dola na kupata idadi kubwa ya majimbo na hata kushika dola."

Anasema, awali wananchi walijiunga na vyama vya siasa kwa kufuata mkumbo au siasa za kishabiki bila tafakuri na kutojua tafsiri itikadi ya chama anachokitaka, kutozisoma sera na mwelekeo wa chama anachokitaka hakuwezi kumfanya awe mwanachama mtiifu na muaminifu.

#### USHINDI WA KWANZA

NCCR- Mageuzi ilishinda baadhi ya majimbo ya uchaguzi kwenye mikoa mbalimbali yakiwamo ya Rorya, Bunda, Musoma Vijijini na Mwibara mkoani Mara, Ubungo Dar es Salaam.

Mengine ambayo chama kilishinda ni Arusha Mjini, Arumeru Mashariki mkoani Arusha, Siha, Vunjo, Moshi Mjini, Moshi Vijijini mkoani Kilimanjaro, Urambo Mashariki mkoani Tabora, Iringa Mjini, Mbeya Mjini na Muleba Kaskazini mkoani Kagera.

Lakini kwa sasa chama hicho kimeporomoka hadi kubaki na mbunge mmoja James Mbatia (Vunjo) mkoani Kilimanjaro, ambaye pia ni mwenyekiti wa taifa wa chama hicho.

Mbatia anakaririwa na gazeti moja la Kiswahili wiki iliyopita, akisema, tangu awali msingi wake katika dhana ya kukubalika kisiasa na kuungwa mkono, ulitegemea zaidi nguvu ya hoja badala ya hoja zenye nguvu.

Kwamba chama kinapigania utu na usawa wa binadamu, haki za wananchi, wajibu walionao kwa Tanzania na kuwafanya mioyo yao iamini na kujali utaifa na uzalendo badala ya migawanyiko au kujengeka kwa matabaka.

> Tumefanya utafiti wa masuala ya kisiasa, uongozi na demokrasia, tumepata majibu yanayotokana na maswali magumu waliyonayo Watanzania, hivyo wananchi sasa wameanza kutuelewa, wanajiunga na chama chetu

#### KILIPOTOKA

Chama hiki kina historia ndefu, kwani mwaka 1989 harakati za kuanzishwa kwake zilitangazwa mbele ya waandishi wa habari jijini Dar es Salaam na mjumbe wa kamati ya uhamasishaji wa NCCR-Mageuzi Mashaka Chimoto, (marehemu) kwamba Tanzania inahitaji mabadiliko ya katiba ili kutoa mwanya wa vyama vingi vya kisiasa kuanzishwa.

Mara baada ya kutangaza azma hiyo akiwa na Prince Bagenda, Ndimara Tegambwage na baadhi ya wazee na watu wengine, kilichofuatia ni kuanzishwa rasmi Kamati ya Mageuzi ya Katiba ya NCCR.

Hatua hiyo iliungwa mkono na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) wakiongozwa na mwakilishi wao Anthony Komu, lakini hata hivyo walikuwa wakihofia kukamatwa na vyombo vya dola.

Aidha walifuatia, kina James Mbatia, Ludovick Bazigiza, Matiku Matare na Mosena Nyambabe, wakiongozwa na wanazuoni kama Dk. Ringo Tenga, Prof. Mwesiga Baregu, Dk. Sengondo Mvungi na Dk. Masumbuko Lamwai (marehemu).

Ili kuweka mambo sawa, waliwatafuta wazee wenye hekima wawe nao katika kamati hiyo wakiwamo Abdalah Fundikira, Balozi Kasanga Tumbo, Kasela Bantu na Lifa Chipaka ili wakivamiwa dunia ijue kwa haraka zaidi.

Kamati hiyo ilikuwa na jukumu la kuitisha na kufanikisha mkutano wa taifa wa wanaharakati wa mageuzi wa vyama vingi na kuhudhuriwa na watu zaidi ya 3,000 walaiokuwa wakidai mabadiliko.

Lakini kutokana na NCCR kutokuwa na taasisi inayojulikana kuitisha mkutano, walitafuta njia ya kukwepa kizingiti hicho na kuanzisha Tanzania Legal Education Trust ambayo ilitisha na kudhamini mkutano huo.



James Mbatia, akiwajibika jukwaani.

Kutokana na mazingira hayo, Rais wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, alilazimika kuunda Tume ya Jaji Nyalali ili kuuliza Watanzania kama wapo tayari kuafiki kuanzishwa kwa vyama vingi nchini au la.

Majibu ya tume hiyo yalikuwa ni kwamba wengi wengependa kiendelee chama kimoja hawakuhitaji vyama vingi, lakini serikali ikaamua kuruhusu kuwapo kwa mfumo wa vyama vingi nchini.

Julai mwaka 1992 vyama vingi vya siasa vikaanzishwa, huku Mabere Marando akichaguliwa kuwa mwenyekiti wa muda NCCR-Mageuzi, akaidhinishwa rasmi mwaka 1994, ikiwa ni moja ya hatua za kuendeleza mageuzi nchini.


Mwaka 1995 mara baada ya Augustine Mrema kujing'atua CCM, uongozi wa chama ulishauriana kumkaribisha na kumpa uongozi ili kuongeza nguvu ndani ya NCCR-Mageuzi na hivyo yeye kubakia kuwa katibu mkuu wa chama.

Ujio wa Mrema ndani ya chama hicho uliongeza nguvu kutokana na kwamba alikuwa tayari amejijengea umaarufu akiwa CCM, hivyo 'akazoa' wafuasi wengi waliomfuata NCCR- Mageuzi.

Mbatia anaamini kwamba sasa ni wakati wa chama hicho kurudi kwenye chati kama kilivyokuwa na msisimko enzi zake kisiasa mwanzoni mwa mwaka 1990 na baada ya mwaka 1995.

Baadhi ya wanasiasa wakiwamo wabunge wameshatangaza kujiunga na chama hicho mara baada ya bunge kuvunjwa, huku chenyewe kikiendelea kupokea wanachama wapya kutoka mikoa mbalimbali.

# Hatua kujiangalia Rais Uhuru, Ruto kukwepa Kenya ya 2007



Mahasimu Raila Odinga (kushoto) pamoja na William Ruto, wakiwa jukwaani kwenye moja ya mikutano ya kisiasa. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mashaka Mgeta**

NI wanasiasa wawili waliokulia ndani ya kilichokuwa chama tawala nchini Kenya almaarufu Kenya African National Union (Kanu), wakiwa washirika wa karibu wa aliyekuwa rais wa pili, hayati Daniel arap Moi.

Rais Uhuru Kenyatta na Makamu William Ruto, wamekuwa na historia hiyo, ingawa wakati wa kuelekea uchaguzi mkuu wa 2007, wawili hao walitengana kisiasa, wakajikuta kwenye kashfa na hatimaye tuhuma za kuchochea machafuko na mauaji ya wakati wa vurugu za baada ya uchaguzi huo.

Uhuru alikuwa upande wa Rais wa zamani Mwai Kibaki wakati Ruto alikuwa mshirika muhimu n wa karibu wa kinara wa upinzani nchini humo, Raila Odinga.

Hata hivyo, matokeo ya uchaguzi mkuu wa 2007 yaliyompa ushindi wenye utata Kibaki wa PNU (kambi ya Uhuru) dhidi ya Odinga wa ODM (kambi ya Ruto) uliibua machafuko yaliyosababisha Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Jinai (ICC) iliyopo Hague nchini Uholanzi, kuwaona wawili hao kuwa na mashitaka ya kujibu dhidi ya mauaji, uharibifu wa mali na kuwasababishia maelfu ya Wakenya kuyakimbia makazi yao na kuwa wakimbizi wa ndani.

Uhuru na Ruto walikuwa miongoni mwa washukiwa sita wa awali waliotajwa na Mwendesha Mashitaka wa ICC kw wakati huo, Louis Moreno Ocampo na hivyo kuwafanya wakijulikana zaidi kama 'Ocampo Six'.

Hatua kwa hatua, washitakiwa hao walianza kupunguzwa hadi kubakia watatu wakiwamo Uhuru, Ruto na mwanahabari, Joshua arap Sang. Uhuru alikuwa anakabiliwa na mashitaka matano, yakiwamo mauaji, ubakaji na kuwafukuza watu kwenye makazi yao kwa madai ya kupanga ghasia za baada ya uchaguzi wa Kenya mnamo mwaka 2007 hadi 2008, ambapo zaidi ya watu 1,200 waliuawa na wengine 600,000 kukosa makazi.

> Sababu nyingine ni baba mzazi wa Gideon Moi, alisimama kidete kuhakikisha kwamba aliyestahili kuiongoza Kenya baada ya kustaafu kwake ni Uhuru na akawania urais, ingawa alishindwa na Kibaki.

Kundi lililodaiwa kulengwa zaidi ni waliokuwa wakipinga ushindi wa Kibaki, hasa wa kutoka jamii ya Wakalenjing anapotokea Ruto na Wajaluo maeneo anapotokea Odinga. Pia Ruto alikabiliwa na tuhuma za uhalifu dhidi ya ubinadamu, lakini akielekezwa zaidi dhidi ya watu jamii ya Wakikuyu anapotokea Uhuru.

Katikati ya kadhia hiyo, iliundwa tume ya usuluhishi iliyoongozwa na Katibu Mkuu wa zamani wa Umoja wa Mataifa Koffi Annan (marehemu) ambayo hata hivyo, Ruto aliyekuwa katika ujumbe wa ODM ya Odinga na Martha Karua wa PNU ya Kibaki waliondolewa kutokana na misimamo yao mikali .

Hata ilipoundwa serikali ya umoja wa kitaifa yakiwa ni matokeo ya usuluhishi, Odinga alitakiwa kuwa Waziri Mkuu na pande zote mbili zilipaswa kumtoa Naibu Waziri Mkuu. Ruto alitarajiwa kuchukua nafasi hiyo kutokea ODM, hasa kutokana na ushiriki wake mpana katika uchaguzi Mkuu huo, kama ilivyokuwa kwa Uhuru wa PNU ya Kibaki.

Kibaki alimpeleka Uhuru katika wadhifa huo, lakini katika jambo ambalo halikutarajiwa, ODM ya Odinga walimteuwa aliyekuwa Mbunge wa Sabatia, Musalia Mudavadi.

Hatua hiyo inatajwa kumkera Ruto na wafuasi wake kwa madai kuwa mwanasiasa huyo 'anayejua kuzichanga karata za siasa za Kenya' alifanikisha kuwaingiza wabunge wengi na kura nyingi za urais kwa Odinga ikilinganishwa na Mudavadi.

Hata Uhuru na Ruto walipofikishwa ICC dhidi ya machafuko ya kisiasa, Odinga akiwa Waziri Mkuu aliweka wazi msimamo wake wa kupinga waliokuwa wanakosoa hatua ya mahakama hiyo, huku wakitaka Kenya ijitoe kwenye uanachama wake.

Upande wa Kibaki akiwa Rais na kwa kumtumia zaidi aliyekuwa Makamu wake, Kalonzo Musyoka, walitafuta kuungwa mkono ili wawili hao wasishitakiwe na Kenya ijitoe ICC. Haikuwezekana.

Kuanzia mwishoni mwa 2011, wanasiasa hao wakaongeza kasi ya ushirikiano wao na karibu kila mwisho wa wiki, walifanya mikutano tofauti wakisisitiza kuwa hawana hatia .

Miongoni mwa mikutano iliyowaleta pamoja ni ule uliofanyika mwaka 2012 katika jimbo la Ikolomani, magharibi mwa Kenya , Ruto alisisitiza nia yao kuwania urais katika uchaguzi wa 2013, na kwamba mgombea mmoja kati yake na Uhuru ndiye angeungwa mkono dhidi ya Odinga, akimwita 'Bwana Vitendawili'.

Akiwa Ikolomani, Ruto alisema ana uhakika kati yake na Uhuru, mmoja wao angeshinda urais, na kusisitiza kuwa kwa namna yoyote, mrithi wa Kibaki asingekuwa Odinga anayejulikana pia kwa majina ya Agwambo, Tinga ama Baba.Ndivyo ilivyokuwa Uhuru alishinda dhidi ya Odinga. Sasa wakati taifa hilo likielekea kwenye uchaguzi mkuu, linashuhudia wanasiasa hao walioungamishwa kwa 'chuki za kisiasa' wamefarakana, huku Uhuru akionyesha kufungamana na Odinga.

Tangu waliposhikana mkono kwa tukio lililo maarufu kama 'hand shake' na kushindwa kwa kambi ya Ruto katika kura ya mabadiliko ya katiba yaliyolenga kupunguza ukubwa wa serikali, Uhuru na Odinga wamekuwa 'wakitembea njia moja' katika hoja na shughuli nyingi za kisiasa na maendeleo nchini humo, Ruto akiachwa.

Lakini kama ilivyo kawaida kwa siasa za Kenya, taarifa za hivi karibuni zimevuja zikimhusisha Uhuru 'kubadili gia angani', akitaka kutoka kwa Odinga kuelekea kwa Gideon Moi, mtoto wa hayati Daniel arap Moi ili awe mrithi wake.

Kwa siasa za Kenya, suala hilo linawezekana kutokana na sababu kadhaa; mosi, Gideon anatoka kwenye chama cha Kanu kilichoasisiwa na baba mzazi wa Uhuru, hayati Jomo Kenyatta aliyekuwa Rais wa kwanza wa Kenya. Hivyo, utawala wa Kenya ukirejea kwenye chama hicho, inatafsiriwa kuwa sehemu ya kumuenzi baba yake.

Pili, Gideon anatoka kwenye jamii ya Wakalenjing walio wengi miongoni mwa wapiga kura wa Kenya. Kwa mujibu wa Tume Huru ya Mipaka na Uchaguzi ya Kenua (IEBC), ukanda wa bonde la Ufa wanapopatikana watu wengi wa jamii ya Wakalenjing ni maeneo yenye wapiga kura wengi nchini humo, kama ilivyo kwa ukanda wa kati na maeneo ya Mlima Kenya wenye Wakikuyu wengi.

Ukanda wa Nyanza anapotokea Odinga una wapiga kura wasiofikia wingi wa wale wa bonde la Ufa ama ukanda wa Kati na mlima Kenya.

Ingawa hali iko hivyo, ni wazi kwamba jitihada za kuwatoa Wakenya katika maslahi ya kisiasa na kiutawala yanayojikita kwenye ukabila na ukanda zikifanikiwa, takwimu hizo zitakosa maana katika kubashiri matokeo ya uchaguzi mkuu ujao.

Sababu nyingine ni baba mzazi wa Gideon Moi, alisimama kidete kuhakikisha kwamba aliyestahili kuiongoza Kenya baada ya kustaafu kwake ni Uhuru na akawania urais, ingawa alishindwa na Kibaki.

Vyovyote iwavyo, uhusiano wa Uhuru na Ruto kwa sasa hautoi hisia za wawili hao kuwa pamoja, ingawa katika siasa za Kenya, lolote linaweza kutokea kwa wakati wowote.

Lakini iwapo Uhuru na Ruto hawatakuwa pamoja katika uchaguzi huo, nini itakuwa hatima ya wafuasi na watu wa jamii zao hasa kambi ya Ruto na Wakalenjing, walioamini kwamba baada ya Ruto kumuunga mkono Uhuru mara mbili, angestahili kuwania urais, lakini inaonekana sasa hawaivi?

Vitendo kadhaa vya Uhuru vimeonyesha kuzidi kujitenga zaidi na Ruto, likiwemo tukio la hivi karibuni la kubadili viongozi wa chama tawala cha Jubilee, huku wanaoaminika kuwa kwenye kambi ya Ruto 'wakipigwa chini.'

Je, mfumo huo wa 'kuwashughulikia' walio karibu na Ruto unaweza kuwa wa manufaa kwa Uhuru dhidi ya Ruto, mwanasiasa mwenye uzoefu na aliyepitia mikikimikiki mingi ya kisiasa, akiishinda?

Pamoja na hisia nyingi zinazoelezwa kwa hali ya kisiasa ilivyo nchini Kenya, wawili hawa wanapaswa kutambua walipotoka hasa uchaguzi mkuu wa 2007, wasiingize Kenya kwenye kadhia nyingine ya kisiasa kama ile ya baada ya uchaguzi huo.

Wanasiasa hao wanaweza kutofautiana kwa namna yoyote katika kutafuta mamlaka ya utawala nchini humo, lakini hawapaswi kuwa sababu ya kuwagawa Wakenya waliorejea katika umoja .

***Maoni: 0754- 691540, mgeta2000@yahoo.com.***



## Wito kutowabagua wagonjwa wa ukoma

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

JAMII imetakiwa kutowanyanyapaa wagonjwa wa ukoma kwa sababu ugonjwa huo hautokani na laana au mikosi kama baadhi ya watu wanavyofikiri, bali ni kama magonjwa mengine.

Ombi hilo lilitolewa na Mkurugenzi wa Shirika la lisilo la kiserikali lenye makao makuu yake jijini hapa la Stigma Within Leprosy Disabilities Should Be Stoped (Lfsc) Trust, Dk. Phillemon Ulunga, wakati alipozungumza na Nipashe jana.

Dk. Ulunga aliwaomba wananchi kutowanyanyapaa walemavu wa ugonjwa wa ukoma kwa sababu ugonjwa huo hautokani na laana au adhabu ya Mungu kama wengine wanavyofikiri, bali ni ugonjwa wa kawaida na unatiba yake.

"Ukoma ni ugonjwa ambao umekuwapo tangu zamani za kale duniani kote, ni ugonjwa unaosababishwa na vimelea aina ya mycobacterium leprae ambapo binadamu huambukizwa kwa njia ya hewa na sio kwa kugusana," alisema.

Alisema ugonjwa huo tiba yake imeshapatikana mgonjwa akiwahi hospitali.

Alibainisha kuwa mgonjwa akipima na kugundulika kuwa na maambukizo au dalili za ugonjwa huo na kuwahi matibabu mapema hatapata ulemavu wa viungo kama wengine wanaochelewa kufika hospitali.

Aidha, alisema shirika hilo linajihusisha kupigania haki za wenye ulemavu wa ukoma na lilianzishwa mwaka 2002 na mmoja wa vijana kutoka familia zilizoathiriwa na ugonjwa huo.

Pia alisema shirika hilo kwa kushirikiana na wahusika wa ugonjwa huo katika maeneo yao wamekuwa na utaratibu wa kuanzisha miradi endelevu ya kilimo, ufugaji uvuvi ili kuondoa utegemezi.

Shirika hilo linafanyakazi mkoani hapa katika wilaya za Chamwino vijiji vya Chinoje na Ng'ailezi, Wilaya ya Bahi vijiji vya Chiguluka na Kigwe na upande wa Wilaya ya Dodoma ni kijiji cha Hombolo.

**"Ukoma ni ugonjwa ambao umekuwapo tangu zamani za kale duniani kote, ni ugonjwa unaosababishwa na vimelea aina ya mycobacterium leprae ambapo binadamu huambukizwa kwa njia ya hewa na sio kwa kugusana," alisema.**

# Corona yafuta maadhimisho Siku ya Mazingira Duniani

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

SERIKALI imefuta maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ambayo ilitarajiwa kufanyika Juni 5, mwaka huu, kitaifa mkoani Lindi, ili kuepusha mikusanyiko inayoweza kusababisha kueneza maambukizo mapya ya virusi vya corona.

Hayo yalibainishwa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira (Mussa Zungu), wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jijini hapa.

Alisema kutokana na hali ilivyo sasa nchini, serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wamekubaliana kuwa maadhimisho ya Wiki ya Siku ya Mazingira Duniani, yatafanyika kwa njia ya vyombo vya habari pamoja na mitandao ya kijamii.

"Vyombo vya habari pamoja na mitandao ya kijamii vitatumika katika kuelimisha na kuhamasisha jamii kutunza mazingira na kuzingatia njia mbalimbali za kujiepusha na maambukizo ya ugonjwa wa corona," alisema Zungu.

Aidha, alisema kuwa kila mkoa utafanya shughuli za maadhimisho hayo kwa kutumia vyombo vya habari vilivyopo kwenye maeneo yao pamoja na mitandao ya kijamii kwa kuzingatia kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu.

"Ikiwa ni pamoja na mashindano ya kuaandika isha zinazohusu kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, hotuba za viongozi, ujumbe mbalimbali kwenye mitandao ya simu pamoja na mikutano ya kitaalamu kuhusu mabadiliko ya tabianchi kwa kuzingatia njia mbalimbali za kujiepusha na virusi vya corona," alisema Zungu.

Alisema Taifa, hivi sasa linakabiliwa na changamoto kubwa ya uharibifu wa mazingira unaotokana na matumizi yasiyoendelevu ya rasilimali za kimazingira.

Alisema, baadhi ya changamoto hizo ni uharibifu wa ardhi, ufyekaji na uharibifu wa misitu, uharibifu wa vyanzo vya maji, uharibifu wa makazi ya viumbe wa majini na upotevu wa bioanuai.

"Changamoto hizi kwa ujumla zinasababisha athari kubwa katika masuala ya kiuchumi na kijamii," alisema.

Pia alifafanua kuwa katika kukabiliana na changamoto hizo serikali kwa kushirikiana na wadau imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kupambana na hali hiyo.

Vilevile, alisema kutokana na mabadiliko ya tabianchi hivi karibuni mafuriko yaliyokumba mkoa wa Lindi, yalisababisha hasara kubwa takribani vijiji 16, viliathiriwa pamoja na watu 19, kupoteza maisha.

"Aidha, takribani watu 1,500 wamekosa makazi pamoja na uhaba wa chakula na kuathiriwa na magonjwa mbalimbali ya mlipuko," alisema Zungu.



Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, akikabidhi zaidi ya Sh. milioni tano kwa Diwani wa Mnadani, Farida Mbarouk, zilizookolewa na taasisi hiyo kutokana na ubadhirifu uliofanywa katika ujenzi wa ofisi ya kata hiyo. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# CHF yazilipa hospitali mil. 496/- huduma wanachama

**Na Renatha Msungu, Dodoma**

MFUKO wa Bima ya Afya ya Jamii (CHF) umelipa Sh. milioni 496 katika hospitali mbalimbali kwa ajili ya matibabu ya wanachama wake ambao wamejiunga na mfuko huo ulioboresha huduma zake.

Mpaka sasa zaidi ya wanachama 280, 000 wamejiunga na CHF ambao huduma zake zimeboreshwa zaidi tofauti na ilivyokuwa awali.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa Dk. Francis Lutalala, mratibu wa CHF jijini hapo alisema fedha hizo zimelipwa ili wanachama wake wanapofika hospitalini wasipate tabu ya kurejeshwa bila kupata matibabu.

Alisema fedha hizo ni za kuanzia Julai mwaka jana hadi mwaka huu, ambapo utaratibu wao huwa wanalipa kabla ili wateja wao wasisumbuliwe wanapofika kupata huduma ya afya.

"Tumeshalipa fedha zote ambazo zinahitajika katika hospitali zote ambazo wagonjwa wanatakiwa kwenda kutibiwa," alisema Dk. Lutalala.

Alisema lengo lao ni kuona hakuna malalamiko kuhusiana na huduma ambazo wao wanatakiwa kuwapa wananchi katika masuala mazima ya matibabu kiafya.

Alisema hivi sasa wanajiandaa kutumia msimu wa mavuno kwa ajili ya kwenda kuhamasisha watu kukata bima hiyo, ambayo wanaamini itawasaidia kwa kiasi kikubwa katika kuhakikisha wanapata matibabu bora.

Alisema watapita katika maeneo mbalimbali, lakini kwa kuzingatia kuepuka mikusanyiko ambayo imekatazwa na serikali kwa ajili ya kujikinga na ugongwa wa corona.

Alisema lengo lao ni kuona kila Mtanzania anakuwa na bima ya afya ambayo ni muhimu kila mmoja kuwa nayo ili aweze kujilinda afya yake pale anapokuwa na uhitaji wa kutibiwa.

Alisema walishafanya kampeni wilayani Mpwapwa, Chamwino na kwingine, na kwamba wanatarajia kwenda kuwapa elimu ya nini maana ya mtu kuwa na bima ya afya iliyoboreshwa.

Dk. Lutalala alisema mtu akiwa na CHF kila mahali anaweza kwenda kutibiwa tofauti na ilivyokuwa awali, ambapo alikuwa anapata matibabu katika mkoa ambao umekata bima hiyo.

Alisema wamepanga kutumia msimu wa mavuno kwenda maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuwashawishi wananchi waweze kujiunga na mfuko huo.





## Matumizi mazuri mitandao kijamii yazidi kuhimizwa

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WATANZANIA wameshauriwa kuitumia mitandao ya kijamii kwa ajili ya kufanya biashara na kujiingizia kipato badala ya kuitumia kuandika matusi na kusambaza vitu, ambavyo havina faida kwao na kwa jamii.

Ushauri huo ulitolewa juzi na wajasiriamali wadogo jijini Mbeya ambao ni wanachama wa mtandao wa wajasiriamali wa Naza Group walipokuwa wakizungumza na Nipashe kuhusiana na namna mitandao ya kijamii inavyowasaidia kutangaza na kuuza bidhaa zao kipindi hiki cha ugonjwa wa Covid-19.

Wajasiriamali hao walidai mitandao ya kijamii ina faida kubwa endapo itatumika vizuri, na kwamba inasaidia kwani haichukui muda mwingi, hivyo kuwafaa hata waajiriwa kuanzisha biashara na kuziendesha bila kuingilia muda wa waajiri wao.

Mwanzilishi wa Mtandao huo, Nazarena Myenzi, alisema yeye ni mwajiriwa, lakini anautumia muda wake wa ziada kufanya biashara kwa kuzitangaza kupitia kwenye mtandao huo kwa ajili ya kujiongezea kipato.

"Nilianza na watu 50, lakini mpaka sasa mtandao huo umetimiza miaka miwili ukiwa na wanachama 500, wakiwamo watumishi wa umma ambao pia ni wajasiriamali na wanauza bidhaa tofauti," alisema Myenzi.

Alisema awali alikuwa anautumia mtandao huo kutangaza bidhaa zake pekee, lakini baadaye akaamua kuwashawishi na wenzake kuanzisha biashara na wengi wakaitikia.

Alisema walibaini kuwa asilimia 70 ya wajasiriamali biashara zao huwa zinakufa baada ya mwaka mmoja tangu wanapozianzisha kutokana na mtandao wa wateja, na kwamba ndio maana waliamua kuanzisha utaratibu wa kuinuana.

Naye Janeth Mgeni alisema mara nyingi Watanzania huwa wanaitumia mitandao kama sehemu ya kupotezea muda na kuongea vitu ambavyo havina msaada, hivyo akawashauri kubadili fikra kwa kuitumia mitandao hiyo kibiashara.

Alisema vijana ndio kundi kubwa ambalo linatumia zaidi mitandao na ndilo kundi linaloweza kufanya vizuri endapo litatumia vizuri mitandao hiyo.

Alisema kabla hajajiunga na mtandao huo alikuwa anafanya biashara yake ya upambaji wa shughuli mbalimbali, lakini alikuwa anafanya na watu wake wa karibu ambao anafahamiana nao, lakini mtandao umemsaidia kupanua wigo wa wateja.

Alisema mbali na kwamba Watanzania wengi hawaitumii vizuri mitandao, lakini pia wanajikuta wakikumbana na mkono wa sheria hasa baada ya serikali kutunga sheria ya makosa ya mtandaoni.

# Ajiua kwa risasi kushindwa kurejesha mil. 100/- za benki

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

MFANYABIASHARA wa madini na mbao katika Mtaa wa Ibala, Kata ya Uyole jijini Mbeya, amejiua kwa kujipiga risasi mdomoni na kutokea utosini kwa kutumia bunduki yake, baada ya kushindwa kurejesha mkopo wa shilingi milioni 100 aliouchukua benki.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, Ulrich Matei, alisema jana kuwa Mei 18, mwaka huu majira ya usiku, mfanyabiashara huyo, Jonas Mahenge (52), aliamua kujipiga risasi kwa kutumia bastola aina ya Browning yenye namba za usajili 00099307.

Alisema Mahenge alikuwa mfanyabiashara wa mbao, mabanzi na viazi na pia alijihusisha na uchimbaji madini Chunya.

Matei aliongeza kuwa hivi karibuni aliomba mkopo katika Benki ya CRDB wa shilingi milioni 100, lakini marejesho ya fedha hizo yalimtatiza akaamua kuuza nyumba yake na kupunguza deni hilo.

Alisema baadaye benki ilimpa sharti la kurejesha mkopo huo kila mwezi shilingi milioni tatu, kitu ambacho alishindwa kutokana na biashara ya madini aliyokuwa akiifanya Chunya ambako alikuwa anapeleka fedha mara kwa mara bila kupata faida.

"Usiku wa Mei 18, mwaka huu familia waliamka usiku saa nane kwa ajili ya kujifukiza kutokana na magonjwa mbalimbali, lakini wakati wenzake wakiwa wameamka na kwenye maandalizi, yeye alirudi na kujifungia ndani akachukua silaha yake na kujipiga risasi mdomoni ikatokea kisogoni na utosini," alisema Matei.

Kamanda Matei alitoa pole kwa familia ya Mahenge na wafanyabiashara wote wa Mbeya kwa msiba huo, huku akishauri wananchi kuwa na mpango mkakati wakati wa kufanya shughuli za kiuchumi kabla ya kuchukua mkopo wowote.

Aliwashauri watu wote kabla ya kufanya biashara yoyote kuwashirikisha wataalamu wa biashara kwa ushauri ili washauri mapato na matumizi ya biashara zao.

Katika hatua nyingine, Jeshi la Polisi limemtia nguvuni, Marko Kandonga (78), mkazi wa Kilambo, Kata ya Njisi wilayani Kyela kwa tuhuma za kupatikana na nyara za serikali bila kibali.

Kamanda Matei alizitaja nyara hizo ni ngozi moja ya mnyama aina ya komba, ngozi ya nyoka aina ya chatu na mkia wa ngiri, ambazo thamani yake haijapatikana.



Wachuuzi wakinadi bidhaa zao kwa abiria katika stendi kuu ya mabasi ya Nanenane, iliyopo jijini Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Chadema yapuuza kuhama kwa viongozi na wanachama

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo Chadema (Chadema), Mkoa wa Mbeya, kimesema licha ya hama hama ya viongozi na wanachama, lakini kiko imara na kitaendeleza siasa safi ambazo zitawapatia ushindi kwenye uchaguzi mkuu ujao.

Hayo yalielezwa jana na Mwenyekiti wa Chadema Mkoa, Joseph China, wakati akizungumza na Nipashe juu ya mustakabali wa siasa mkoani humo licha ya hamahama ya viongozi na wakereketwa wa chama hicho.

Alisema suala la kuhama kwa wafuasi wa chama hicho ni la kawaida kwa kuwa nao mwaka 2015 walivuna wanachama wengi kutoka vyama vingine vya siasa.

Alidai wakati huu chama kiko imara kuliko kipindi kingine kwani kila aliyekuwa na nia ovu kwa sababu ya mfumo uliopo, anajiengua mwenyewe.

"Chadema hatubabaishwi na hii hama hama ya wabunge, madiwani wala wafuasi wengine... chama ni maarufu kuliko mtu, wanaondoka waondoke sisi wengine tunabaki ili tuendelee kuwatumikia wananchi," alisema China.


Akizungumzia uchaguzi ujao, China alisema chama kitakuwa makini kuwasimamisha wagombea makini na wasio wanafiki kwa sababu tayari wamejifunza na kuwatambua wasaliti.

Alisema hawatakubali kurubuniwa na yeyote ambaye atahamia Chadema na kupewa madaraka badala yake watawasimamisha wagombea wenye mapenzi mema kwa chama.

Aliongeza kuwa bado wana imani kwa Jimbo la Mbeya Mjini kwa sababu bado viongozi wake wa kuchaguliwa wananchi wanawahitaji.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Jacob Mwakisole, alisema kazi nzuri alizozifanya Rais John Magufuli ni kampeni tosha, hivyo chama hicho kitashinda kwa kura nyingi.

Alisema shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwamo ujenzi wa vituo vya afya, zahanati, huduma za maji, soko la madini na mambo mengi ambayo Rais Magufuli ameyafanya, yamejenga matumaini kwa wakazi wa mkoa huo.



# Wawakilishi waja juu mitandao kuwachafua watu urais 2020

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

BAADHI ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamesikitishwa na tabia ya baadhi ya watu wanaotumia vibaya mitandao ya kijamii kuwachafulia majina viongozi wengine kwa kuwahusisha katika kinyang'anyiro cha urais wa Zanzibar.

Mwakilishi wa kuteuliwa na Rais, Juma Ali Khatib, alisema amesikitishwa na tabia za baadhi ya watu kutumia vibaya mitandao ya kijamii kurusha taarifa za viongozi wengine na kuwahusisha na mbio za urais kwa kuwachafulia majina.

Alisema hizo ni kampeni mbovu ambazo zinakwenda kinyume cha ustaarabu wa tabia za watu wa Zanzibar kwa kusingiziana na kutoleana kashfa.

Alizitaka taasisi zinazoshughulikia masuala ya mitandao ya kijamii kulifanyia kazi suala hilo na kuona tabia hizo zinakomeshwa kwa sababu sio utamaduni wa harakati za vyama vya siasa.

"Nimesikitishwa na tabia za baadhi ya watu wanaoitumia vibaya mitandao ya kijamii kuwakashifu viongozi wengine kwa hofu ya kisingizio mbio za urais," alisema.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mohamed Aboud, alisema tabia inayofanywa na baadhi ya watu wakiwamo wanasiasa kuwachafulia majina viongozi waliopo serikalini katika hatua zinazoonekana mbio za urais ni sawa na hofu za kisiasa na woga.

Alisema serikali inalifahamu suala hilo na vyombo vya ulinzi ikiwamo Jeshi la Polisi na mitandao ya mawasiliano ya simu wameachiwa na kulifanyia kazi.

Alieleza kuwa watu wanaochafuliwa majina yao ni wale viongozi pekee kutoka katika Chama Cha Mapinduzi (CCM), kitendo ambacho kinaonekana kufanywa makusudi ikiwa sehemu ya mikakati ya hofu ya uchaguzi.

"Tumeshuhudia wapo watu wanatumia vibaya mitandao ya kijamii kwa kuandika majina ya viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuwahusisha na uchaguzi mkuu, huku wakitaja kasoro zao na udhaifu wao katika siasa na ushiriki wa wananchi katika kuleta maendeleo," alisema.

Katika siku za hivi karibuni baadhi ya mitandao ya kijamii imekuwa ikichapisha majina ya viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na kuwahusisha na uwezekano wa kugombea nafasi ya urais wa Zanzibar, huku wakitoa udhaifu wao na kuwahusisha na matukio ambayo hayawahusu.



Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Said Hassan (kulia), akijadiliana jambo na Mwakilishi wa Jimbo la Paje, Jaku Hashim Ayoub, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakikishi, Mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# JPM afagiliwa kufungua utalii

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wamempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano, John Magufuli, kwa uamuzi wake wa kutaka baadhi ya shughuli muhimu za maendeleo ikiwamo sekta ya utalii kuendelea kufanya kazi kwa ajili ya kukuza uchumi na pato la wananchi.

Mwakilishi wa Jimbo la Amani, Rashid Ali Juma, alisema kauli za Magufuli zimewatia moyo wananchi wengi na sekta muhimu ya utalii kwa kutaka kuona kwamba shughuli hizo zinarudi katika siku za hivi karibuni kwa sababu janga la ugonjwa wa corona limeanza kudhibitiwa.

Juma alisema hayo wakati akichangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka wa fedha 2020-2021 katika Baraza la Wawakilishi.

Alisema Zanzibar ni miongoni mwa nchi ambayo imeathirika vibaya katika sekta ya utalii, ambayo huingiza fedha za kigeni kwa asilimia 80 kutokana na kusitishwa kwa shughuli za uingizaji wa wageni.

"Naunga mkono kauli ya Rais Magufuli ya kurudisha shughuli za utalii ikiwamo kuingia kwa ndege zitakazobeba wageni kwa sababu kwa kiasi kikubwa tumefanikiwa kudhibiti ugonjwa wa corona...na sisi kwa upande wetu tunatakiwa kuanza kufanya maandalizi ya aina hiyo," alisema.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Konde, Omar Seif Abeid, alisema wakati umefika sasa kwa kamisheni ya utalii kujiweka sawa kwa maandalizi ya kuanza kufanya mawasiliano ya safari za watalii kuja nchini.

Alisema ugonjwa wa corona usitumike kusitisha shughuli za maendeleo na kukuza uchumi, ambapo cha msingi ni kuchukua kila aina ya tahadhari kupambana na ugonjwa huo.

"Nimefurahishwa na hotuba ya Rais Magufuli yenye kutoa moyo ya kuwajenga kimawazo Watanzania kujipanga kufanya shughuli zetu za maendeleo na kiuchumi, hivyo ugonjwa wa corona usitumike kukwamisha mikakati ya maendeleo," alisema.

Naye Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, aliipongeza Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale kwa kufanya kazi kubwa ya kuinuwa sekta ya utalii ya ukarabati wa majengo ya kale pamoja na magofu.

Alisema utalii wa mambo ya kale ndio utaivusha Zanzibar katika miaka ijayo kwa kuwawezesha watalii wenye hadhi kuja na kuona historia ya mambo ya kale.

"Nimefurahishwa na mikakati ya wizara katika malengo ya kuimarisha utalii wa mambo ya kale yakiwamo magofu ambayo hutumiwa na watu mbalimbali kujua historia ya mambo ya kale na watawala wake," alisema.

Hivi karibuni Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, alipotembelea eneo la Hospitali ya Rufani eneo la Binguni Wilaya ya Kati Unguja, alisema serikali inakusudia kuanza kupunguza masharti ya ugonjwa wa corona, ikiwamo kufungua shule baada ya ugonjwa huo kudhibitiwa kwa kiwango kikubwa.

## Wakumbushwa ujazaji fomu maadili uongozi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi na viongozi wengine wametakiwa kujaza fomu za maadili ya viongozi wa umma.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Utumishi wa Umma na Utawala Bora), Haroun Ali Suleiman, alisema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akitoa ufafanuzi kuhusu suala la ujazaji wa fomu za viongozi na maadili pamoja na mali zao.

Alisema suala la viongozi kuwataka kujaza fomu za tamko la mali zao ni la kisheria na limetajwa katika katiba ikiwa ni sehemu ya kutekeleza dhana ya utawala bora.

Alisema tamko la kutaja mali na kuorodhesha linawahusu viongozi wote ikiwamo wa ngazi za kitaifa akiwamo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein.

"Mheshimiwa Spika, napenda kuwakumbusha baadhi ya viongozi kuanzia wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, mawaziri na wale wateule wote wa rais na baadhi ya watumishi wa umma kwamba tunalazimika kujaza fomu za tamko la mali kwa mujibu wa sheria...mtumishi atakayeshindwa kutekeleza agizo hilo ajue atakuwa amekiuka sheria," alisema.

Alieleza kujaza fomu za maadili na mali za viongozi ni muhimu ili serikali iweze kuwafahamu viongozi wake juu ya utaratibu wa kupata mali wanazomiliki.

Alisema haiwezekani kwa mtumishi wa umma anaajiriwa, lakini katika kipindi cha miaka miwili tu anamiliki mali nyingi bila ya kuzitolea maelezo yake anapotakiwa kufanya hivyo.

"Tunataka kila mtumishi wa umma tunapomwajiri kujua mali zake, lakini akiwa katika utumishi tujue pia kama amepata mali nyingine kwa njia zipi... atujulishe katika maelezo yake," alisema.

Alisema utaratibu huo unatumika katika nchi zote ambazo zinaongozwa kwa njia ya kidemokrasia ikiwamo Tanzania, kwa lengo la kuweka uwazi wa matumizi ya fedha za umma.

Tume ya maadili ya viongozi wa umma imeundwa kwa mujibu wa sheria NO.4 ya mwaka 2015 ambapo miongoni mwa majukumu yake ni kupokea na kusajili na kuhakiki tamko la mali na madeni kutoka kwa viongozi wa umma.

Pia kupokea malalamiko hufanya uchunguzi kuhusu uvunjaji wa sheria ya maadili ya viongozi kwa hatua za kinidhamu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## TANGAZO LA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

MAULID ABDALLAH MVUGILIJE MKAZI WA NDALA SHINYANGA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YAKE YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI T. 557 BDC KIBOKO, CHASSIS NAMBA LFFWJ09C592F01527 ENGINE NAMBA 156FM1962211938, AMBAYO ILIPOTEA MWAKA 2020 MAENEO YA NDALA SHINYANGA

KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA MAULIDI ABDALLAH MVUGILIJE

KWA SIMU NAMBA 0735184879 RB NAMBA SHY/RB/2020, CONTROL NAMBA 9910812686617

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Meshack Abinel Magenge anatangaza kupotelewa na kadi ya gari Aina ya Fuso yenye namba za usajili T 797 BZC. Chasis No. FK619K522059. Engine No. 6D17855009 rangi Silver Yellow.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo Cha polisi. Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/372928/2020.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA BUKOBA
HATI YA KUITWA SHAURINI (SUMMONS)

Shauri la rufaa jinai/ madai/ mirathi/ taraka namba............. 3/2020 Mahakama ya wilaya ya Bukoba.
Jina ALLAN MWOMBEKI MUTASINGWA .............APPLICANT
Dhidi ya
Jina WILLBARD MUTASINGWA.............RESPONDENT
Kwa WILLBARD MUTASINGWA
K.K...........

Elewa kuwa kesi ya rufaa hiyo hapo juu itatajwa/ itasikilizwa/ kusomewa hukumu tarehe 28/05/2020 asubuhi katika mahakama ya wilaya Bukoba. Hivyo unapaswa kuhudhuria bila kukosa.

Hati hii imetolewa na kutiwa mhuri wa mahakama leo tarehe 30/04/2020

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA WILAYA BUKOBA

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
Kuitwa Shaurini Mdaiwa
Katika Mahakama ya mwanzo..Dodoma mjini
Wilaya ya Dodoma
Talaka nambari 35/2009

Mdai: Arafa Issa
Mdaiwa: Adamu Ibrahimu
Kwa: Adamu Ibrahimu Chang'ombe
Kwa kuwa mdai/wadai ameleta madai yake kwamba : Madai ya Nyumba
Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku 21/05/2020 saa 02:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri Hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohisu shauri Hilo kwa ajili ya kujitetea katika shuri Hilo.

Na Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibisha Kama umepokea kuitwa Shaurini hii, utaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii Leo tarehe 19/25/2020.

PRIMARY COURT
URBAN DODOMA

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku
Tupigie 0782253676
Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Makamu wa Rais na mkewe wapata corona

**JUBA,** Sudan Kusini

MAKAMU wa Rais wa kwanza wa Sudani Kusini, Riek Machar na mkewe, Angelina Teny, wamethibitishwa kuambukizwa virusi vya corona.

Machar alisema kwamba yeye na mke wake ambaye pia ni Waziri wa Ulinzi, wamepata maambukizo baada ya kutangamana na jopo la ngazi ya juu la kukabiliana na virusi hivyo nchini humo. Machar amesema hana dalili zozote na hali yake ya afya iko sawa lakini atajiweka karantini kwa siku 14.

Wengine waliothibitishwa kuambukizwa ni walinzi kadhaa na wafanyakazi. Mpaka sasa Sudan Kusini imerekodi waathirika 236 na vifo vine hiyo ni kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na ofisi yake.

Wiki iliyopita maofisa walitangaza kwamba virusi hivyo vimefikia kwenye kambi ya waliotoroka makazi yao ambao wamekuwa wakiutaka Umoja wa Mataifa uwalinde katika mji mkuu wa Juba tangu 2013. **BBC**

## Waziri Mkuu wa Lesotho ajiuzulu

**MASERU,** Lesotho

THOMAS Thabane ametangaza kuwa atajiuzulu kama Waziri Mkuu wa Lesotho kufuatia miezi kadhaa ya shinikizo baada ya kutajwa kama mshukiwa katika mauaji ya aliyekuwa mkewe.

Hakusema ataachia madaraka lini lakini chama chake kimesema kuwa Waziri Mkuu mpya ataapishwa leo.

Mke wa Thabane wa sasa (mke mdogo), ambaye alikuwa akiishi naye wakati aliyekuwa mkewe anauawa, alishitakiwa mwezi Februari kwa kuhusishwa na mauaji hayo. Thabane mwenye miaka 80, na mkewe mdogo wamekanusha kuhusika na mauaji ya mke mkubwa.

Lesotho imeghubikwa na ukosefu wa uthabiti wa kisiasa mwaka huu na waziri huyo mkuu alipoteza wingi wa viti bungeni wiki jana pale muungano unaomuunga mkono uliposambaratika na serikali mpya inatarajiwa kushika usukani Ijumaa hii.

Wanaume waliokuwa wamejihami kwa silaha walimpiga risasi na kumuua Lipolelo Thabane. **BBC**

# Marekani yajiondoa WHO mchango kifedha

**NEWYORK,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amemtumia barua Mkuu wa Shirika la Afya Duniani, (WHO) akitishia kuondoa kabisa mchango wa taifa lake kifedha kwa shirika hilo, kutokana na janga la Covid-19.

Barua hiyo imeipa WHO siku 30 kufanya maboresho makubwa au ipoteze mamilioni ya dola na hata uanachama wa Marekani kwa pamoja. Barua iliyoelekezwa kwake Mkuu wa WHO, Tedros Adhanom Ghebreyesus, inakosoa awamu mbalimbali za WHO za kushughulikia janga la corona tangu mwezi Desemba.

Bwana Trump pia amelituhumu shirika hilo la Umoja wa Mataifa (UN) kuwa kibaraka wa China.

Rais huyo anayekabiliwa na uchaguzi mwaka huu na yeye kukosolewa kwa namna anavyoshughulikia janga hilo, ameitupia lawama China kwa kujaribu kuficha taarifa kuhusu mlipuko wa virusi vya corona pia ameishutumu WHO kuwa kushindwa kuiwajibisha China.

**China itatoa Dola bilioni 2 katika kipindi cha miaka miwili ili kusaidia mataifa duniani na kutoa ombi la kugawanya chanjo itakapokuwa tayari.**

Awali Waziri wa Afya wa Marekani pia aliitupia lawama WHO kuruhusu Covid -19 kushindwa kudhibitika kwa gharama ya maisha ya watu wengi.

"Shirika hili lilifeli kupata habari ambayo ulimwengu ulihitaji", alisema waziri wa Afya wa Marekani, Alex Azar.

Alazar alitoa matamshi hayo katika hotuba kwenye mkutano wa UN. Mkuu wa WHO awali alikubali kufanyika uchunguzi ambao utaweka wazi jinsi shirika hilo lilivyoangazia mlipuko huo.

Dk. Tedros amesema kwamba uchunguzi huru ambao utatazama mafunzo na kutoa mapendekezo utafanyika mapema.

Mkutano huo wa siku mbili unaofanyika kila mwaka na unaohusisha nchini 194 wanachama wa WHO huangazia kazi ya shirika hilo na unajiri wakati ambapo kuna vita vya maneno kati ya China na Marekani kuhusu virusi hivyo.

Trump, ambaye anakabiliwa na uchaguzi mkuu mwaka huu ambaye amekosolewa jinsi anavyotatua ugonjwa huo nchini Marekani, amelaumu China kwa kujaribu kuziba mlipuko huo na kuilaumu WHO kwa kushindwa kuiwajibisha China.

Rais wa China Xi Jingpin, ambaye ametetea vitendo vya China wakati wa mlipuko huo, alisema katika mkutano huo kwamba taifa lake lilikabiliana na ugonjwa huo kwa uwazi na kusisitiza kwamba uchunguzi wowote ufanyike baada ya mlipuko huo kudhibitiwa.

Aliongezea China itatoa Dola bilioni 2 katika kipindi cha miaka miwili ili kusaidia mataifa duniani na kutoa ombi la kugawanya chanjo itakapokuwa tayari.

Wakati huohuo Rais wa Korea Kusini Moon Jae-in amesema WHO inafaa kupewa uwezo wa kisheria kuhakikisha kuwa mataifa yanaripoti milipuko na kupeana data. **BBC**



Mkuu wa WHO, Tedros Adhanom Ghebreyesus. **PICHA: MTANDAO**

# Trump ataja dawa ya kujikinga virusi vya corona

**NEWYORK,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amesema kwamba anakunywa dawa ya hydroxychloroquine kujikinga dhidi ya virusi vya corona ingawa maofisa wa afya wametoa onyo juu ya usalama wa dawa hiyo.

Akizungumza katika Ikulu ya White House, aliwaambia wanahabari kwamba ameanza kunywa dawa hizo zinazotibu ugonjwa wa malaria na hivi karibuni imetumika kutibu ugonjwa wa ngozi.

"Nimekuwa nikiinywa kwa karibia wiki moja na nusu sasa na niko hapa, bado niko hapa," hilo lilikuwa tangazo lake la kushangaza.

Hakuna ushahidi unaoonesha kwamba dawa ya hydroxychloroquine ina uwezo wa kukabiliana na virusi vya corona na wataalamu wanaonya kuwa inaweza kusababisha matatizo ya moyo.

Rais huyo, mwenye miaka 73, alikuwa ameitisha mkutano kwa ajili ya kuzungumzia sekta ya migahawa jumatatu wiki hii, aliposhitukiza wanahabari kwa kuwafahamisha kwamba amekuwa akinywa dawa hiyo.

"Utashangaa ni watu wangapi wanaokunywa dawa hii, hasa wafanyakazi waliomstari wa mbele katika kukabiliana na janga la virusi vya corona kabla ya wewe kuipata, wahudumu wa afya, wengi wao tu wanakunywa dawa hii, Mimi pia ninainywa." Trump alisema.

Alipoulizwa kuhusu faida za kunywa dawa ya hydroxychloroquine, Trump alisema anapigiwa simu nyingi sana zinazosifu dawa hii hiyo na kwamba amesikia mengi mazuri kuhusu dawa hiyo ya hydroxychloroquine na ikiwa siyo nzuri, ataawaarifu kwamba hakuridhika.

Ingawa kuna baadhi ya watu waliothibitishwa kupata maambukizo ya virusi vya corona, Rais alisema tena Jumatatu kwamba hana dalili zozote na huwa anapimwa kila wakati.

Pia aliongeza kwamba amekuwa akinywa dawa mbadala ya madini ya zinc na pia alikunywa dawa ya azithromycin, ambayo matumizi yake ni kuzuia maambukizo ya kuua bakteria mwilini.

Alipoulizwa ikiwa daktari wa Ikulu amependeeza yeye kuanza kunywa dawa hiyo ambayo bado inazua utata katika matumizi yake dhidi ya virusi vya corona, Trump alisema yeye mwenyewe ndiye aliyeomba kupewa dawa hiyo.

Dk. Sean Conley, Daktari wa Rais, alisema katika taarifa iliyotolewa na Ikulu Jumatatu baadae kwamba Trump alikuwa katika hali nzuri kiafya na hana dalili zozote za virusi vya corona.

Shirika la Usimamizi wa Chakula na Dawa la Marekani mwezi uliopita lilitoa ushauri na kusema dawa ya hydroxychloroquine haijathibitishwa kuwa salama wala yenye ufanisi.Pia shirika hilo lilionesha kwamba dawa hiyo inaweza kusababisha matatizo makubwa ya ugonjwa wa moyo kwa wagonjwa wa Covid-19. **BBC**

# BECKHAM: BADO 'NAMISI' SANA SOKA



**NEW YORK,** Marekani

DAVID Beckham amesema bado analikosa sana soka wakati akiwa amefikisha miaka saba tangu astaafu kutoka kwenye mchezo huo.

Nahodha huyo wa zamani wa England alicheza mechi yake ya mwisho akiwa Paris Saint-Germain kwenye Ligue 1 dhidi ya Brest, Mei 18, 2013.

Kutambua namna 'alivyomisi' soka, Beckham aliposti video wakati wa nyakati zake za kuvutia ikiwamo ushindi wa Manchester United kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 1999 pamoja na ujumbe kwenye Instagram.

Beckham ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 45, haamini kama umepita muda mwingi tangu aondoke kwenye kucheza soka na bado ana kumbukumbu wakati akicheza, huku kwa sasa nia yake ikiwa ni kuwekeza kwenye umiliki wa klabu yake mpya ya Ligi Kuu ya Marekani (MLS), Inter Miami.

"Siamini ni miaka saba leo tangu nimecheza mechi yangu ya mwisho ya ushindani kama mwanasoka wa kulipwa," aliandika.

"Ni kumbukumbu ya kuvutia. Nilikuwa na bahati kucheza na wachezaji wenzangu na kushabikiwa na mashabiki. Bado namisi sana. "Siwezi subiri ukurasa mpya hapa Inter Miami."

Katika miaka yake 21 ya uchezaji wa soka la kulipwa, Beckham pia alizicheza Real Madrid, LA Galaxy na AC Milan kwa nyakati tofauti.

# Rais PSG asifia nguvu ya ajabu ya Ronaldo




**PARIS,** Ufaransa

"NGUVU ya ajabu" ya Cristiano Ronaldo imesifiwa na Rais wa Klabu ya Paris Saint-Germain, Nasser Al-Khelaifi.

Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or, Ronaldo ni wa mataji ya ligi akiwa na Manchester United, Real Madrid na sasa klabu ya Juventus.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 35, pia ameshinda mataji matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya - mara nne akiwa na Madrid na moja wakati akiwa pale United, huku akiisaidia Juve kushinda taji la Serie A na Supercoppa Italiana msimu uliopita.

Awali alihusishwa na mabingwa wa Ligue 1, PSG, na Al-Khelaifi amemsifia Ronaldo wakati uvumi huo ukiendelea.

"Mwaka mmoja baadaye, anaonyesha nguvu ya ajabu, na uwezo wa hali ya juu kabisa," alisema Al-Khelaifi akiliambia Jarida la France Football.

"Bado amebakia kuwa na hamasa na hamu ya kuimarika kila siku na mara zote anajisukuma kusonga mbele.

"Napenda nia yake ya kutochoka; yeye ni mfano mzuri sana kwa wanamichezo wote kwa siku za usoni."

Ronaldo amefunga mabao 21 kwenye Serie A katika mechi 22 na 25 katika mashindano yote kabla ya kusimama kwa michezo kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

# Hazard katika mizani Real Madrid

**MADRID,** Hispania

EDEN Hazard anahitaji kuufanyia kazi zaidi mwili wake ili aweze kupona kabisa kifundo cha mguu na kuiwakilisha tena Real Madrid msimu huu.

Madrid wiki iliyopita walirudi kwenye kambi yao ya mazoezi pale Valdebebas kwa mara ya kwanza baada ya miezi miwili, baada ya michezo yote duniani kufungwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Wachezaji walifanya mazoezi binafsi kwa vipindi maalumu kabla ya kufanya kwa makundi juzi Jumatatu, wakati Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, ikitarajiwa kurudi katika hali ya kawaida.

Hazard hajacheza tangu Februari 22, baada ya kuvunjika kifundo cha mguu wakati walipofungwa 1-0 dhidi ya Levante, maana yake amecheza mechi 15 tu kwa Madrid tangu alipojiunga nayo akitokea Chelsea kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 100 mwaka jana.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alionekana kufurahia kuanza mazoezi na wachezaji wenzake, lakini alionekana anahitaji kufanya kazi ya ziada ili apone kabisa na kuwa tayari kurudi uwanjani.

"Najisikia vizuri sana kurudi uwanjani na kujifua na wachezaji wenzangu," alisema Hazard akiiambia Real Madrid TV.

"Sasa natakiwa kusubiri kwa ajili ya mechi zije, lakini nina furaha sana. Baada ya miezi miwili nje nahitaji kufanya kazi ya ziada ili niwe na nguvu ya kucheza mpira.

"Nataka kuwa tayari kwa ajili ya mchezo unaokuja.

"Kwa sasa mazoezi ni bora, tunaweza kujifua tunavyotaka. Wiki ya kwanza itakuwa ni ngeni, lakini tunaweza kufanya mazoezi kwa makundi na pia kushambulia goli.

"Tunataka kuwa wote pamoja na kujaribu kufanya kazi kama kundi."

Rais wa LaLiga, Javier Tebas ana matumaini mashindano hayo yatakuwa tayari kurudi Juni 12, mwaka huu.



# MESSI HAWEZI KUONDOKA BARCELONA – MORATTI



**MILAN,** Italia

RAIS wa zamani wa Inter Milan, Massimo Moratti amesema Lionel Messi hataondoka Barcelona, huku pia akizungumzia majaliwa ya nyota wa Nerazzurri hao, Lautaro Martinez.

Messi amekuwa akihusishwa na Inter tangu Moratti aliposema mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or kujiunga na klabu hiyo ya Serie A si "ndoto isiyoruhusiwa."

Nyota huyo wa Barca, Messi ana mkataba na mabingwa hao wa LaLiga hadi mwaka 2021, lakini majaliwa yake yanaonekana kutokuwa mbali na Camp Nou, ambako alikwaruzana na wajumbe wa bodi msimu huu.

"Messi ni mchezaji wa ndoto ya kila mtu, lakini hawezi kuondoka Barcelona. Yeye bado ni mchezaji bora pale," alisema Moratti akiiambia Gr Parlamento.

Mshambuliaji huyo wa Inter, Martinez amekuwa akihusishwa na mpango wa kujiunga na mchezaji mwenzake kwenye kikosi cha Argentina, Messi pale Barcelona.

Pia alikuwa akihusishwa na miamba wa Hispania, Real Madrid na Manchester City ya Ligi Kuu ya England, na Martinez amefunga mabao 16 katika mechi 31 kwenye mashindano yote kabla ya mlipuko wa virusi vya corona.

"Itategemea na yeye mwenyewe, nimesoma kwamba, Barcelona wanaandaa ofa ya nguvu kwa ajili yake ambayo itakuwa ngumu kwake kusema hapana," alisema Moratti.

# Serie A inaweza kuanza Juni 15

**ROME,** Italia

LIGI Kuu ya Italia, Serie A, itaendelea kusimama angalau hadi Juni 14, mwaka huu Shirikisho la Soka la Italia (FIGC), limethibitisha.

Ligi hiyo ya Italia ilisimama tangu Machi 9, mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Kulikuwa na matumaini kwamba itarejea tena Juni 13, huku Klabu zikiwa tayari zimeanza mazoezi Jumatatu wiki hii. Hata hivyo, ligi hiyo sasa haitaweza kuanza hadi Juni 15, mwaka huu.

Maamuzi ya FIGC yamekuja baada ya Serikali ya Italia kutangaza kuruhusu klabu kuanza mazoezi ya pamoja Jumatatu wiki hii, huku zikitakiwa kuzingatia kanuni za kujikinga na maambukizo ya corona.

"Serie A sasa italazimika kusubiri hadi Juni 14 ili kurejea tena, huku tukiangalia namna ya kujilinda na virusi vya corona," ilisomeka taarifa ya FIGC.

Bingwa mtetezi Juventus walikuwa wanaongoza kwa pointi moja dhidi ya Lazio kileleni mwa msimamo wakati ligi hiyo ikisimamishwa.





# Werner njia nyeupe Inter

**MUNICH,** Ujerumani

MSHAMBULIAJI wa Klabu ya RB Leipzig, Timo Werner ana uwezekano mkubwa zaidi wa kujiunga na Inter Milan wakati akihusishwa na Liverpool, kwa mujibu wa gazeti la Calciomercato.

Huku Liverpool wakiwa wanaonekana kuwa na nafasi nzuri zaidi ya kumsajili Werner, mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani sasa ni wazi kwamba anaweza kuhamia Inter.

Nyota huyo wa RB Leipzig ameripotiwa kuwaniwa na klabu kubwa kama vile Manchester United, Chelsea na Bayern Munich.

Werner amekuwa akipewa nafasi kubwa zaidi kujiunga na Liverpool inayonolewa na kocha, Jurgen Klopp, lakini sasa karata inaonekana kuiangukia Inter.

Wakati nyota wa Inter, Lautaro Martinez akiwa anawaniwa kwa udi na uvumba na Barcelona, Werner anaonekana kuwa anaweza kuwa mrithi wake pale San Siro.

Kwa mujibu wa ripoti kutoka Ujerumani na Italia, Werner mwenyewe anaonekana kwamba yupo tayari kwenda Inter kuliko Liverpool.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HUDSON-ODOI MATATANI AKITUHUMIWA KUBAKA

●●● Polisi wamtia nguvuni England, Chelsea yagoma kuongea lolote huku...

**LONDON,** England

WINGA wa Chelsea na England, Callum Hudson-Odoi alikamatwa kwa kuhusishwa na madai ya ubakaji mapema asubuhi ya Jumapili iliyopita na sasa ameachiwa kwa dhamana.

**Polisi waliitwa kwenye mtaa mmoja jijini London baada ya mwanamke mmoja kupiga siku kwamba amebakwa.**

Na polisi walimchukua mwanamke huyo na kumkimbiza hospitali, huku Hudson-Odoi mwenye umri wa miaka 19, akikamatwa katika eneo la tukio na aliachiwa baadaye kwa dhamana.

Na ametakiwa kurudi tena polisi katikati ya Juni mwaka huu kwa ajili ya kupata maelezo ya kina zaidi.

Hata hivyo, klabu yake ya Chelsea imekataa kuzungumzia lolote kutokana na tukio hilo.

Ripoti nyingine zinadai kwamba mwanamke huyo anayedai kubakwa, alimtembelea mwenyewe Hudson-Odoi.

Hudson-Odoi, ambaye ameichezea timu ya Taifa ya England mechi tatu, Septemba mwaka jana alisaini mkataba wa miaka mitano kuichezea Chelsea, na alikuwa mchezaji wa kwanza wa Ligi Kuu ya England kupimwa na kukutwa na maambukizo ya virusi vya corona.

Amepona na sasa kama ilivyo kwa wachezaji wengine wa Chelsea anasubiria kurudi kwenye mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na kumalizia msimu wa ligi.

## ZISIKUPITE

### KAI KUITOSA LIVERPOOL

KIUNGO mshambuliaji wa Bayer Leverkusen, Mjerumani, Kai Havertz mwenye umri wa miaka 20, anatakiwa kuipiga chini nafasi ya kujiunga na Liverpool na achague kwenda Borussia Dortmund, amesema mchezaji wa zamani wa Ujerumani, Jens Nowotny. ***(Goal)***

### MARTINEZ AKARIBIA BARCA

BARCELONA wamepiga hatua zaidi kwenye mpango wao wa kumsajili mshambuliaji wa Inter Milan na Argentina, Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 22 na Pjanic. ***(Mundo Deportivo)***

### UNITED WAMRUDIA KOULIBALY

MANCHESTER United wapo tayari kufufua mpango wao wa kumuwania mlinzi wa Napoli raia wa Senegal, Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 28, baada ya kuona Liverpool imeonyesha nia ya kumhitaji. ***(Gazzetta dello Sport via Daily Express)***

### LAZAZO NJIAPANDA NEWCASTLE

WINGA Valentino Lazaro aliyeko kwa mkopo Newcastle United anasubiria kumsikia Mkurugenzi, Lee Charnley wapi majaliwa yake yatakuwapo msimu ujao. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 raia wa Austria alijiunga na hapo Magpies kutoka Inter Milan Januari. ***(Newcastle Chronicle)***

### POCHETTINO RUKSA KIBARUANI

KOCHA Mauricio Pochettino raia wa Argentina yupo huru kusaini klabu yoyote baada ya mkataba wake na Tottenham kumalizika rasmi. ***(Telegraph)***

### TOTTI NA STORI YA ROMA

GWIJI wa AS Roma na Italia, Francesco Totti mwenye umri wa miaka 43, amesema alikaribia kujiunga na Real Madrid, lakini hawakumpa ofa kubwa kama ya mshambuliaji wao, Raul. ***(Libero via Marca)***

### SILVA KUJIFUNGA CITY

KLABU ya Manchester City inajiamini David Silva mwenye umri wa miaka 34, atakubali kuongeza mkataba mfupi ili kumruhusu kiungo huo kumalizia msimu uliobaki. Kiungo huyo wa kimataifa wa Hispania anatarajia kuondoka Juni 30, mwaka huu wakati mkataba wake utakapomalizia. ***(ESPN)***

### UNITED KUMUITA KIPA WAO

MANCHESTER United inapanga kumuita tena kipa wa Ureno mwenye umri wa miaka 23, Joel Pereira kutoka anakocheza kwa mkopo pale Hearts bada ya ligi kuu ya Scotland kutokana na kufutwa rasmi msimu huu. ***(Manchester Evening News)***

### CHELSEA KUWAFUNGA NYOTA

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard ana matumaini wachezaji wake ambao mikataba yao inakaribia kumalizika mwishoni mwa msimu huu, watasainishwa ya muda mfupi. Mikataba ya kiungo wa Brazil, Willian mwenye umri wa miaka 31, na mshambuliaji wa Ufaransa, Olivier Giroud mwenye miaka 33, mikataba yao inamalizika Juni 30, mwaka huu. ***(Chelsea)***

### KARIUS KUTORUDI MAZOEZINI

GOLIKIPA wa Liverpool, Loris Karius mwenye umri wa miaka 26, hatarudi kwenye mazoezi na klabu. Raia huyo wa Ujerumani amevunja mkataba wake wa mkopo na klabu ya Besiktas mapema mwezi huu. ***(Daily Star)***

# HABARI MICHEZO

## Bigirimana akiri Yanga kumtaka

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Namungo FC, Mrundi Bigirimana Blaise, ameweka wazi kuhusu uongozi wa Yanga kumfuata na kuhitaji huduma yake kwa msimu ujao.

Akizungumza na Nipashe jana kwa simu, Blaise alisema baada ya viongozi hao kufika kwake naye aliwaelekeza kwa meneja wake anayemsimamia.

Alisema aliwataka kuwasiliana na meneja wake kwa sababu bado yupo ndani ya mkataba na timu ya Namungo.

"Ni kweli Yanga walikuja na nikawapa maelekezo ya kuonana na meneja wangu, hivyo wao ndio wanazungumza, kwa sasa naheshimu muda wa mkataba wangu uliobaki na Namungo," alisema Blaise.

Alisema alisaini mkataba wa mwaka mmoja na umebaki muda mfupi kabla ya kumalizika msimu huu na kwamba atatoa kipaumbele kwa mabosi wake wa sasa wakati wa kufanya maamuzi ya timu atakayoitumikia msimu ujao.

"Namungo tulianza mazungumzo ila bado hatujaafikia muafaka kutokana na hili janga la corona, ila nina imani hivi karibuni tutarejea kukamilisha ligi na kuendelea kuzungumza na viongozi," alisema Blaise.

Alisema kikubwa anachoangalia ni maslahi kama Yanga watatoa dau analolihitaji ataenda endapo Namungo wakishindwa kupata muafaka.

## Zimamoto yapania ubingwa Ligi Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LICHA ya kushika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar, Kocha Mkuu wa timu ya Zimamoto, Juma Abrahamani Said, amesema ana matumaini makubwa ya kunyakuwa ubingwa wa ligi hiyo endapo itarejea tena baada ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19).

Zimamoto ipo nafasi ya nne katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama 42 na tayari wakati huu ikiwa imeshacheza mechi 20, ikiwa imeshinda michezo 12, sare sita na kupoteza miwili.

Akizungumza na gazeti hili jana, Said alisema licha ya ligi hiyo kusimama, lakini wachezaji wake wanaendelea kufanya mazoezi kwa nafasi zao hivyo hayo na anaamini maandalizi tosha ya kuhakikisha wanachukua ubingwa.

Alisema amekuwa akiwapatia programu za mazoezi kwa mchezaji mmoja mmoja kulingana na nafasi yake ili kujiweka tayari na maamuzi yanayosubiriwa kutoka serikalini endapo ligi hiyo itaendelea ama la.

Aidha, alisema kikosi chake hicho kimejipanga kufanya mashambulizi katika michezo iliyobaki ili lengo lao la kuwa bingwa litimie.

Akizungumzia kuhusu sare mfululizo alizozipata kabla ya ligi hiyo kusimama, alisema hiyo imetokana na kuwakosa wachezaji wake wa kikosi cha kwanza ambao walikuwa katika mafunzo ya Kijeshi (Depo), lakini kwa sasa wamemaliza na tayari walishaungana na timu kabla ya mlipuko wa corona.

# NAHIMANA: NATAKA KUICHEZEA SIMBA

**Na Saada Akida**

KIPA namba moja wa KMC FC na timu ya Taifa ya Burundi, Jonathan Nahimana amesema malengo yake sasa angependa kujiunga na Simba kwa msimu ujao baada ya kumaliza mkataba wake na timu yake hiyo.

**Kipa huyo alisema mambo mengi yameshawishi kutamani kucheza ndani ya kikosi cha 'Wekundu wa Msimbazi' hao, ikiwamo suala la wachezaji wa klabu hiyo kulipwa vizuri.**

Alisema malengo yake ni kucheza timu kubwa msimu ujao, kutokana na msimu huu kuonyesha kiwango kizuri ambacho kinakidhi kufikia kile anchokitarajia.

"Sitaweza kuongeza mkataba KMC, malengo yangu ni kubadili mazingira, kama nitabaki katika kikosi hicho basi itabidi waongeze dau la usajili na mshahara," alisema Nahimana.

Alisema hakuna kiongozi yeyote wa Simba ambaye amefanya naye mazungumzo, na kwamba hayo ni matamanio yake binafsi kuelekea msimu ujao kuwa miongoni mwa wachezaji wa kikosi hicho.

Aidha, alisema awali kabla ya kutua KMC, kuna klabu zilimfuata ikiwamo Horoya FC ya Guinea, Nkana FC ya Zambia pamoja na Yanga ila ilishindikana kutokana na suala la kimaslahi.

"Yanga tulishindwana katika suala la fedha maana walitaka kunipa ambayo naipata KMC, sikuweza kujiunga nao.

"Kumfuata kocha Ettiene Ndayiragije Azam FC kipindi kile kilishindikana kutokana na kuwapo kwa kipa wa kigeni kutoka Ghana, walinieleza kwamba wasigesajili makipa wawili wa kigeni," alisema Nahimana.

Alisema walimtaka asubiri hadi msimu ujao endapo kocha huyo angeendelea kubaki kukinoa kikosi hicho.

"Kocha ameondoka sasa, kuondoka kwake haitazuia kwenda kupata nafasi endapo watanihitaji," alisema kipa huyo.

**MCHUMA MPYA...**




Basi dogo aina ya Coaster ambalo juzi Kamishna Jenerali wa Magereza nchini, Suleiman Mzee, aliikabidhi timu ya soka ya jeshi hilo, Tanzania Prisons kwa ajili ya matumizi ya safari zake mbalimbali zikiwamo za Ligi Kuu Tanzania Bara iliyosimama kwa sasa kwa sababu ya hofu ya maambukizo ya virusi vya corona (COVID-19). **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Michezo kurejea kwa mafungu*

**Na Faustine Feliciane**

SIKU chache baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kurudia kauli yake ya kufikiria kuruhusu michezo kurejea nchini, Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo imesema wataanza kurejesha mchezo wa soka pekee kabla ya kuruhusu michezo mingine kuendelea.

Akizungumza jana, Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Harrison Mwakyembe, alisema wataruhusu michezo kwa tahadhari kubwa ili kuendelea kujilinda dhidi ya virusi vya corona (COVID-19).

"Hatuwezi kuruhusu michezo yote kwa pamoja, lazima twende kwa tahadhari, tutaanza na soka kwa sababu ni ukweli tunahitaji kupata mwakilishi wa nchi kwenye mashindano ya kimataifa na kuna viporo hivyo tumeona ni vema kuanza na soka kwanza na baadaye michezo mingine itarejea," alisema Dk. Mwakyembe.

Alisema kwa sasa michakato mingine inaendelea kabla ya kuruhusiwa rasmi kurejea kwa michezo na kamati zilizoundwa kufanya tathmini ya namna gani itaendesha michezo pale serikali itakaporuhusu, zinaendelea kufanya kazi yake.

Tayari nchi nyingine zimeanza kurejesha ligi za soka baada ya kusimama kwa muda kutokana na mlipuko wa virusi vya corona vilivyoanzia katika jimbo la Wuhan nchini China kabla ya kusambaa duniani kote.

Mpaka ligi zinasimama Machi 17, mwaka huu, kwenye mbio za ubingwa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ilikuwa inaongoza ikiwa na pointi 71 ikifuatiwa na Azam yenye pointi 54 na Yanga iliyopo mchezo mmoja nyuma baada ya kushuka dimbani mara 27, inashika nafasi ya tatu ikiwa na alama 51.

Michezo
Jumatano Mei 20, 2020
Nipashe



Hudson-Odoi matatani akituhumiwa kubaka UKURASA 22

# Ndemla ondoka Simba- Meneja

## ●●● Aambiwa ni wakati wa kutazama kwingineko ili...

Na Faustine Feliciane

USTAWI wa kipaji cha kiungo wa Simba, Said Hamisi Ndemla, umeendelea kupigiwa kelele na wadau wa soka ambao wanataka kuona mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, akiendelea kupata nafasi ya kucheza na kuwa msaada kwa timu ya Taifa, Taifa Stars, imeelezwa.

**Baada ya wadau wengi kujitokeza kwa nyakati tofauti kumshauri Ndemla kutazama kwingineko nje ya Simba ili kulinda kipaji chake, safari hii aliyekuwa meneja wake, Jamal Kisongo naye amemtaka kiungo huyo kumulika klabu itakayomba nafasi ya kucheza.**

Akizungumza katika mahojiano maalum jijini Dar es Salaam, Kisongo alisema ni wakati wa Ndemla kuamua kuondoka Simba na kwenda kuitumikia timu itakayompa nafasi kwa kuwa ana uwezo wa kucheza popote nje na ndani ya nchi.



Kisongo (pichani) alisema kuwa Ndemla ni mchezaji mzuri katika nafasi yake, lakini kwa bahati mbaya yupo kwenye kikosi chenye changamoto kubwa ya namba kutokana na kuwapo wachezaji wa kigeni wenye uwezo.

"Kiukweli alipo sasa Ndemla si sehemu sahihi..., ni mchezaji mzuri ambaye anaweza akaenda sehemu nyingine kurejesha heshima yake na kiwango alichokuwa nacho huko nyuma, wapo wanaomshauri aendelee kubaki alipo sasa, lakini niwe muwazi kama shabiki wake Ndemla anapaswa kutoka kwenye timu ya sasa na kwenda sehemu nyingine, wakati anatoka Sweden na kurejea Simba alikuwa kwenye kiwango kikubwa sana tofauti na sasa.

"Hakuna sababu ya yeye kuendelea kukaa Simba, ukitazama umri wake unakwenda na ana uwezo mkubwa wa kuhamia klabu nyingine na kupata nafasi, kwangu mimi Ndemla ni bonge la mchezaji ambaye ninamkubali sana," alisema Kisongo.

Ushauri huo wa Kisongo umekuja siku chache baada ya Kiungo wa Yanga Haruna Niyonzima naye kumtaka Ndemla kutazama maisha nje ya Simba ili kulinda kipaji chake badala ya kuendelea kusugua benchi katika klabu hiyo aliyoichezea tangu akiwa kinda.

Lakini pia winga wa zamani wa Simba, Ulimboka Mwakingwe naye hivi karibuni alisema Ndemla anapaswa kuondoka ndani ya klabu hiyo kwa sababu si sahemu rafiki kwa kiwango chake.

Ulimboka alisema Ndemla anapaswa kushtuka na kuchukua uamuzi wa kuondoka hata kwa mkopo mwishoni mwa msimu huu maana amekuwa chini ya makocha tofauti Simba lakini ameishia kukaa benchi.

"Ndemla ana uwezo wa kucheza popote lakini si Simba tena, unajua makocha mara nyingi huangalia wachezaji wa kikosi cha kwanza sasa anapopokea timu kutoka kwa kocha aliyepita na yeye hutoa nafasi kwa wale ambao walikuwa wakicheza hiyo ni dhana iliyopo wazi," Ulimboka alimshauri hivi karibuni.

Lakini kwa upande wa Kocha Msaidi wa Simba, Selemani Matola, hivi karibuni pia alisema suala la Ndemla kupata nafasi si jukumu lake bali lipo chini ya Kocha Mkuu, Mbelgiji Sven Vandenbroeck.

Matola alikiri kuwa Ndemla ni mchezaji mwenye kipaji na si wa kufundishwa, na kwamba licha ya kukosa nafasi Simba, anaamini akichezeshwa mara kwa mara ana uwezo wa kuwazidi baadhi ya nyota wa kikosi cha kwanza.

Kuhusu kutolewa kwa mkopo, Matola ambaye alimfundisha tangu akiwa timu B na kuushauri uongozi kumpandisha kikosi cha wakubwa, alisema hilo ni jukumu la mchezaji mwenyewe na uongozi wa timu anayoichezea.

Ndemla anafahamika kwa uwezo wake mkubwa wa kupiga mashuti ya mbali akitumia 'guu' la kulia na wakati akipata nafasi Simba mara kwa mara baada ya kupandishwa kikosi cha kwanza mwaka 2013, aliitwa kwa mara ya kwanza Taifa Stars Oktoba 12, 2014 na kuichezea dhidi ya Benin.

Kuanzia hapo aliendelea kuitwa Taifa Stars na kuichezea mara 11.



Said Ndemla akijifua ufukweni mwa Bahari ya Hindi jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Yanga SC yazindua Twenzetu Mabadiliko

Na Adam Fungamwango

MWENYEKITI wa Klabu ya Yanga, Dk. Mshindo Msolla, amezindua kampeni ya kuelekea uzinduzi wa mfumo wa mabadiliko ya kiundeshaji kwa klabu hiyo kongwe nchini.

Akizungumza kwenye mtandao rasmi wa klabu hiyo jana, Dk. Msolla alisema kamati hiyo ya mabadiliko itakuwa chini ya kamati ndogo itakayosimamiwa na Mwanasheria Msomi Alex Mgongolwa huku mchakato wote wa mabadiliko ya kimfumo ukisimamiwa na kufadhiliwa na mdhamini mkuu GSM ukiwa na kauli mbiu 'Twenzetu Kwenye Mabadiliko'.

Dk. Msolla (pichani chini) alisema huu ni mwanzo halisi wa kuelekea kuweka sahihi makubaliano hayo ambayo ndiyo itakuwa muda rasmi wa mchakato huo wa mabadiliko kuanza.

"Moja ya dhamira yangu wakati nagombea uongozi ilikuwa ni kubadilisha muundo wa uendeshaji, sasa nadhani ndoto hii inaelekea kukamilika. Ombi langu kwa wanachama wa Yanga tuwe kitu kimoja, tuungane na viongozi tuungane na wadhamini ili tuweze kufanikisha hilo," alisema Dk. Msolla.

Yanga inataka kubadilika kuwafuata watani zao wa jadi Simba ambao tayari wameshaenda kwenye mfumo mpya wa uendeshaji.




GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >